MKOMBOZI
COMMERCIAL BANK
a bank with integrity

## BENKI YA BIASHARA MKOMBOZI

# MKUTANO MKUU WA 16 WA WANAHISA

26 JULAI, 2025

# BODI YA WAKURUGENZI



Bw. Gasper Njuu
Mwenyekiti wa Bodi



Bw. Respige Kimati
Mkurugenzi Mtendaji



Bw. Benedict Sudi
Mjumbe



Bi. Uphoo Swai
Mjumbe



Askofu Mkuu. Beatus Kinyaiya
Mjumbe



Bw. Robert Mtendamema
Mjumbe



Padre Dkt. Charles Kitima
Mjumbe



Bw. Martin Mdoe
Mjumbe

# TIMU YA UENDESHAJI



Bw. Respige Kimati
Mkurugenzi Mtendaji



Bw. Vitalis Michael
Afisa Mkuu wa Fedha



Bw. Thomas Enock
Afisa Mkuu wa Operesheni



Bw. Crispin Kweka
Mkaguzi Mkuu wa Ndani



Bi. Paulina Kunjumu
Mkuu wa Idara ya Sheria



Bw. Wilbert Luoga
Mkuu wa Idara ya Mikopo



Bi. Fortunata Olomi
Afisa Mkuu wa Biashara



Bi. Brenda Fernandes
Mkuu wa Idara ya
Rasirimali Watu



Bw. Daudi Senkondo
Mkuu wa idara
Ukubalifu na
Vihatarishi



Bw. Faraja Augustino
Mkuu wa Hazina



Bw. Leonard Weinand
Mkuu wa Kitengo cha
Tehama na Mifumo

# YALIYOMO


1. Dira ........................................ 1

2 Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka ........................................ 2

3. Taarifa ya Mwenyekiti ........................................ 4

4. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji ........................................ 7

5. Dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Tano ........................................ 10

6. Yatokanayo na Dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Tano ........................................ 31

7. Taarifa ya Wakurugenzi ........................................ 34

8. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu wa Nje na Taarifa za Fedha ........................................ 48

9. Pendekezo la kutoa gawio ........................................ 77

10. Uteuzi wa Mkaguzi Mkuu wa nje ........................................ 77

11. Uchanguzi wa wajumbe wa bodi ........................................ 77



**Kamilisha kila kitu kupitia Mkombozi Wakala kitaani kwako**

- Weka na Toa pesa
- Fungua akaunti
- Lipa bili




MkomboziBankPlc www.mkombozibank.co.tz info@mkombozibank.co.tz

# DIRA NA DHIMA

## DIRA

Kuwa benki inayoongoza katika kushughulikia mahitaji ya ukuaji wa biashara ndogo na za kati kwa kutoa huduma za kibenki zenye viwango vya hali ya juu na kwa uadilifu kwa wateja wote kuanzia wadogo kabisa na kampuni za biashara.

## DHIMA

Kuwa benki itakayotoa huduma za kifedha za viwango vya juu kwa sekta zote na viwango vyote vya uchumi kwa namna ambayo ni endelevu huku ikiwajibika kwa jamii ili kukidhi matarajio ya wadau..



# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA

**Taarifa inatolewa kuwa** Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki ya Biashara Mkombozi utafanyika tarehe **26 Julai, 2025** kuanzia saa tatu asubuhi katika Ukumbi wa Selous unaopatikana ndani ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), maeneo ya Posta, Dar es Salaam.

## AJENDA

1. Kuthibitisha akidi na Kufungua Mkutano;
2. Kupitishwa kwa Ajenda ya Mkutano;
3. Kuthibitisha dondoo za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 15 uliofanyika tarehe 27 Julai, 2024;
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 15 uliofanyika tarehe 27 Julai 2024
5. Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa ya Wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024;
6. Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa ya fedha ya Benki kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 pamoja na kupokea taarifa ya Mkaguzi wa Nje wa hesabu juu ya taarifa hiyo ya fedha;
7. Kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo la Gawio kwa Mwaka 2024;
8. Kuteua Mkaguzi wa nje wa hesabu za Benki;
9. Kuteua Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi;
10. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao;
11. Mengineyo;na
12. Kufunga Mkutano.

## MAELEZO:

1. Mwanahisa anayetaka kuhudhuria Mkutano Mkuu wa mwaka anapaswa kuja na nakala ya stakabadhi ya ununuzi wa Hisa au Cheti cha Hisa cha kumtambulisha kua ni Mwanahisa.
2. Mwanahisa mwenye stahili ya kuhudhuria mkutano huu ana haki ya kumteua mwakilishi wake wa kupiga kura kwa niaba yake kwa mujibu wa taratibu za kampuni. Fomu husika inayopaswa kujazwa na Mwanahisa kwa ajili ya uteuzi huo inatakiwa kufikishwa kwa katibu wa Benki siku tatu kabla ya mkutano. Kwa taasisi, fomu inapaswa kuwa katika lakiri ya taasisi ya Mwanahisa. Fomu hiyo iandikwe kama ifuatavyo.

**Benki ya Biashara Mkombozi**

Mimi/Sisi..................................................................................wa........................................................................., nikiwa/tukiwa Mjumbe/Mwanahisa wa kampuni iliyotajwa hapo juu, ninamteua/tunamteua ..................... ................................ wa ......................................................... ........................................ kama mwakilishi wangu/wetu kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki utakaofanyika terehe 26 Julai, 2025.

Saini .........................................................

Imetolewa leo tarehe.................Mwezi....................2025.

3. Wanahisa wote na/au wawakilishi wao watahitajika kujisajili kwanza kabla ya kuingia kwenye ukumbi siku ya mkutano.

4. Vitabu vyote vilivyo na ripoti za kifedha na taarifa nyingine muhimu za benki vitapatikana kwenye matawi ya Benki na tovuti ya Benki https://mkombozibank.co.tz/ wiki tatu kabla ya mkutano.

Kwa maelezo na taarifa zaidi, wasiliana na Ofisi ya Benki kwa anuani ifuatayo:

Benki ya Biashara Mkombozi,
Kiwanja Namba 40, Nyuma ya Kanisa la Mtakatifu Yosefu,
Mtaa wa Mansfield,
S.L.P 38448,
DAR ES SALAAM.
Namba za Simu: +255 22 2137806/7.
Namba ya bure ya maulizo: 0800 750 040
Barua Pepe: shareholders@mkombozibank.co.tz
info@mkombozibank.co.tz

**PAULINA KUNJUMU**
**KATIBU NA MWANASHERIA WA BENKI**
**KWA MAELEKEZO YA BODI YA WAKURUGENZI**
**JUNE, 2025**

# TAARIFA YA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI.

**Wapendwa Wanahisa,**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninatumia fursa hii kuwakaribisheni nyote katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Sita wa wanahisa wa Benki ya Biashara Mkombozi. Ninaona fahari kuwasilisha kwenu mambo muhimu ya Ripoti ya Mwaka na Taarifa ya Fedha ya Benki kwa mwaka ulioishia Desemba, 2024.

Ninaipongeza Menejimenti ya Benki pamoja na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi kwa bidii na kuwezesha kupatikana mafanikio yaliyoainishwa katika Ripoti hii. Vilevile, ninawashukuru wenzangu, wajumbe wa Bodi kwa kutoa miongozo na uangalizi bora uliofanikisha utekelezaji wa malengo ya Benki. Leo hii ninasimama mbele yenu na kuwasilisha kwenu mafanikio ya Benki kwa mwaka 2024 kutokana na kujitolea bila kuchoka na mchango wa kila mmoja wetu katika kufanikisha malengo ya Benki. Kwa dhati kabisa, ninawashukuru wateja wetu kwa kuendelea kuiunga mkono Benki yetu. Bila wao, Benki isingeweza kuyafikia mafanikio haya. Ninatumia pia fursa hii kuzishukuru taasisi zinazosimamia na kudhibiti sekta ya fedha ambazo ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Serikali na wadau wengine wote ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakiunga mkono na kutoa mwongozo kwa Benki. Kwa wanahisa wetu, ninawashukuru sana kwa kuendelea kuunga mkono na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali mtaji ili kufanikisha malengo ya Benki.

## Mafanikio Makuu ya Mwaka 2024

Wakati matokeo ya kifedha yako katika kurasa 50-56 ya Taarifa ya Mwaka, inaonyesha kwa muhtasari baadhi ya mafanikio ya kimkakati ambayo yamekuwa msingi wa ukuaji wa biashara ya benki:

- Tulitekeleza Mfumo wa shughuli za Kibenki (Core Banking System) mpya na kukamilisha mchakato wa uhamishaji wa shughuli zote za kibenki tarehe 16 Desemba 2024.
- Mradi wa Mfumo wa Usimamizi wa Shule umekamilika na utekelezaji umeanza kwa baadhi ya shule, tukilenga kuandikisha shule 200 ifikapo mwaka 2026.
- Suluhisho za kidijitali zimeendelea kuwa ajenda kuu ya benki. Huduma za Wakala (Mkombozi WAKALA), Mfumo wa Usimamizi wa Matoleo ya Kanisani (SADAKA Digital), huduma za miamala kwa njia ya dijitali zimeendelea kupanuka na kupata mwitikio chanya kwa wateja.

- Tulitekeleza mradi wa kuunganishwa kwa huduma za ATM kati ya benki yetu na NMB Bank Plc kupitia mtandao wa Umoja Switch, hivyo kuwawezesha wateja wetu kutumia mtandao wa ATM wa benki ya NMB.
- Mfumo wa Usimamizi wa Fedha kwa Vyuo umetekelezwa katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT), na mkakati unaendelea kutekelezwa katika taasisi nyingine za elimu ya juu.
- Mfumo wa Usimamizi wa fedha wa Hospitali umekamilika na tayari mchakato wa usajili unaendelea na Hospitali ya Bugando, tukilenga kuusambaza kwa hospitali nyingine katika soko letu la kimkakati.
- Maandalizi yameanza kwa ajili ya kufungua matawi mapya matatu ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025 kama sehemu ya mpango wa upanuzi wa huduma zetu.

Kwa ujumla, juhudi za kuimarisha na kukuza biashara zetu zimeendelea kuzaa matunda kupitia ongezeko la wateja, mapato, usimamizi bora wa gharama na udhibiti thabiti wa vihatarishi.

## Hali ya Uchumi Mwaka 2024

Uchumi wa ndani wa Tanzania uliboreka na kukua kwa 5.6% kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na 5.1% mwaka 2023. Matarajio ya muda na ya kati ni mazuri, ambapo pato la taifa linatarajiwa kukua kwa karibu 6% mwaka 2025, likichangiwa na maboresho ya kimfumo na mazingira bora ya biashara.

Mfumuko wa bei ulibaki katika kiwango cha wastani, ukifunga mwaka kwa asilimia 3% sawa na mwaka 2023, hali inayooana na malengo ya muda wa kati ya taifa na viwango vya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Sera ya fedha ilitekelezwa kwa mafanikio, hali ya ukwasi ilikuwa ya kuridhisha na kulingana na mwenendo wa uchumi. Hatua hizi zilisaidia kuondoa soko la fedha za kigeni lisilo rasmi (la magendo) na kupunguza ubashiri kuhusu kiwango cha ubadilishaji wa fedha.

## Fedha na Mikopo

Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa 14.9% mwaka 2024, kutoka 10.7% mwaka 2023, ukichangiwa na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi na ongezeko la rasilimali za kigeni. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa 16.8%, ikiwa ni miongoni mwa viwango vya juu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kilimo kiliongoza kwa ukuaji wa mikopo kwa 43.5%, kikifuatiwa na madini kwa 36.4%. Mikopo binafsi iliendelea kuwa na sehemu kubwa ya mkopo wote kwa 37.2%.

Viwango vya riba ya mikopo na amana vilibaki takribani sawa na mwaka 2023. Riba ya mikopo ilikuwa karibu 16%, huku mikataba maalum ikiwa na viwango vya wastani wa 13%. Riba ya amana kwa ujumla ilikuwa 8% (kutoka 7.5% mwaka 2023), na kwa wateja wakubwa ilipanda hadi 10%.

### Mpango Mkakati 2024–2025

Benki inaendelea kutekeleza mikakati ya muda mfupi na wa kati kwa lengo la kupata faida endelevu, ukuaji wa biashara na faida kwa wanahisa kupitia mgao wa faida. Tutaendelea kupenya sokoni kwa kutoa suluhisho bora za kifedha na kutumia kikamilifu fursa zilizopo ndani ya soko letu la kimkakati.

### Nyaraka za Mkutano Mkuu

Nyaraka za Mkutano Mkuu wa Mwaka, ambazo tayari zimewasilishwa kwa wanahisa, zinajumuisha Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha ya benki kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2024. Hizi zitawasilishwa rasmi kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Wanahisa mnakaribishwa kuchangia mawazo na mapendekezo kwa mafanikio zaidi ya benki.

**Asanteni sana.**

**GASPER CASMIR NJUU**
**MWENYEKITI WA BODI**
**26 JULAI, 2025**



# TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI

## Utangulizi

Ninafurahi kuwasilisha taarifa ya utendaji wa benki kwa kipindi cha fedha kilichomalizika tarehe 31 Desemba 2024. Timu yetu imeendelea kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha benki inabaki kuwa makini, imara na yenye faida. Tumepiga hatua kubwa katika miaka ya hivi karibuni na mwaka 2024 umeonesha mafanikio zaidi. Tunaendelea kujikita katika kuimarisha biashara yetu na kuongeza mapato kwa njia endelevu.

## Matokeo ya Kifedha

Benki ilifanya vizuri mwaka 2024 kwa kufanikisha malengo yake ya kuongeza uwekezaji, mapato na faida. Jumla ya mali ilikua kwa asilimia kumi (10%) hadi TZS bilioni 282, ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa mikopo na uwekezaji katika masoko ya fedha. Mikopo kwa wateja ilifikia TZS bilioni 162, sawa na ongezeko la asilimia ishirini na moja (21%), huku uwekezaji katika masoko ya fedha ukifikia TZS bilioni 75. Kwa pamoja, maeneo haya mawili yalichangia asilimia themanini na nne (84%) ya ongezeko la mali.

Amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia tano (5%) hadi TZS bilioni 217, ambapo asilimia 68 ya amana hizo ni za gharama nafuu. Ukuaji huu wa kiasi cha kati umetokana na mkakati wetu wa kupunguza utegemezi wa amana za gharama kubwa ili kuongeza faida.

Mapato Halisi yalifikia TZS bilioni 29, yakiwa yameongezeka kwa asilimia kumi na sita (16%). Kati ya hayo, TZS bilioni 21 yalitokana na riba, na TZS bilioni 8.4 kutoka ada na kamisheni. Tulidhibiti gharama kwa ufanisi, ambapo gharama za jumla ziliongezeka kwa asilimia sita (6%) tu hadi TZS bilioni 17.7. Hii ilisababisha uwiano chanya wa gharama dhidi ya mapato wa asilimia hamisini na saba (57%), licha ya kuendelea na uwekezaji wa ndani.

Ubora wa mikopo uliimarika kwa kupungua kwa mikopo chechefu hadi asilimia tatu pointi nane (3.8%) ya mikopo ghafi, ikiwa ni punguzo la asilimia hamsini na tatu (53%). Hii ni kutokana na uboreshaji katika utoaji, ufuatiliaji na usimamizi wa mikopo. Hali hii ilichangia ongezeko la faida kabla ya kodi kwa asilimia thelathini na nne (34%) hadi TZS bilioni 11.5.

Mizania ya benki iliendelea kukua, ambapo faida kwa mtaji wa wanahisa (Return on Equity) ilifika asilimia ishirini na tisa (29%), ikilinganishwa na asilimia ishirini na nane (28%) mwaka 2023. Mtaji wa wanahisa uliongezeka kwa asilimia ishirini na nane (28%) hadi TZS bilioni 40 kutoka TZS bilioni 31 mwaka 2023.

Benki ina mtaji wa kutosha na ukwasi mzuri, ikiwa na msingi mpana na wa kuaminika wa amana. Uwiano wa ukwasi ulifikia asilimia ishirini na nane (28%) dhidi ya kiwango cha chini

cha kisheria cha asilimia ishirini (20%). Uwiano wa Mtaji wa Msingi (Tier 1) ulikuwa asilimia kumi na saba (17%) na Mtaji Jumla (Tier 2) asilimia kumi na nane (18%)— viwango vyote viwili vikiwa juu ya matakwa ya ya asilimia 12.5 na asilimia 14.5 mtawalia.

## Upanuzi na Ukuaji

Tunaendelea kuwekeza katika maeneo yenye faida kubwa na ushindani wa kipekee, huku tukilenga kuongeza upatikanaji wa huduma zetu na kukuza biashara kwa ubora.

Tumepiga hatua nzuri katika utekelezaji wa mkakati wetu wa upanuzi kupitia huduma ya Mawakala wa Benki. Tumesajili jumla ya mawakala 1,377, wakiwemo mawakala 12 wa kimkakati walioko kwenye Parokia. Mawakala hawa wa kimkakati wanaendeshwa na Parokia, huku benki ikisaidia katika kuweka muonekano bora unaoakisi ubora wa huduma za benki yetu katika vituo hivyo. Kadhalika benki inashiriki mikakati ya usajili wa wateja, wafanyakazi na mafunzo katika vituo hivyo. Mpango wa muda mrefu ni kuvigeuza vituo hivi kuwa matawi madogo au vituo vya huduma kulingana na kiwango cha fursa ya biashara kitakachodhihirika.

Huduma ya mawakala hutumika kama mbadala wa tawi rasmi kwa ajili ya huduma za msingi kama kufungua akaunti na kufanya miamala ya kuweka au kutoa pesa. Kupitia njia hii, benki ilifanya miamala ya thamani ya TZS bilioni 108 mwaka 2024.

Sambamba na huduma ya mawakala, tunapanga kufungua matawi ya benki katika maeneo ya kibiashara yenye umuhimu kimkakati, kwa lengo la kuongeza ukuaji endelevu na faida.

Kwa kutambua kuwa huduma za kifedha zinaelekea kidijitali, tumeendelea kuvumbua suluhisho za kidijitali kwa wateja binafsi na wa taasisi. Tumezindua programu ya simu (MKCB App) ili kuendana na huduma ya USSD (*150*06#). Pia tumeanzisha huduma za Usimamizi wa Fedha kwa Taasisi kama vile "Shule Soft" kwa shule na "SADAKA Digital" kwa makanisa na pia suluhisho la huduma za kibenki kwa mahospitali.

Tumeimarisha huduma ya intaneti kwa wateja binafsi na taasisi, ili kuimarisha ushindani wetu sokoni. Ingawa njia hizi zimekusudiwa kuongeza mapato na amana, kipaumbele chetu kikubwa ni ukusanyaji wa amana, ambao ni msingi wa ukuaji wa biashara yetu. Mwaka 2024, benki ilikusanya TZS bilioni 112 kupitia njia za kidijitali. Tumeendelea kushirikiana na kampuni za Fintech kubuni na kusambaza suluhisho za kidijitali ili kupanua ujumuishaji wa kifedha.

## Uwekezaji katika Mfumo wa Kibenki

Ninafurahi pia kuwajulisheni kuwa tumefanikisha uhamishaji wa shughuli zetu kutoka mfumo wa zamani wa kibenki (Br. Net) kwenda mfumo mpya (RUBIKON), kuanzia tarehe 16 Desemba 2024. Uwekezaji huu ni hatua muhimu katika mafanikio na uendelevu wa mkakati wa benki wa ukuaji wa muda mrefu. Mfumo mpya una uwezo mkubwa wa

kiteknolojia na unatuwezesha kujipanga vyema kukuza biashara na kuimarisha huduma zetu kwa wateja siku zijazo.

## Kuwajengea wanahisa thamani

Tunaamini kuwa kwa kuongeza uwekezaji na kulenga maeneo ya kimkakati, tutapanua sehemu yetu ya soko na kuongeza mapato na mizania kwa muda wa kati na mrefu.

Mwaka huu, tumeonyesha dhamira yetu kwa kutoa gawio la TZS 92.4 kwa kila hisa, licha ya mazingira yenye changamoto yanayohitaji uwekezaji na mtaji zaidi kwa ajili ya ukuaji.

Tumejipanga kutoa matokeo chanya kila mwaka kwa wanahisa wetu kupitia:

- ukuaji wa mapato,
- kuboresha ufanisi wa kiutendaji,
- kutumia teknolojia na mifumo ya kisasa kuboresha huduma,
- na kuondoa vikwazo vya kimfumo ili kurahisisha na kufanikisha shughuli zetu kidijitali.

Lengo letu ni kutoa huduma bora zaidi kwa wateja, kuchangamkia fursa za ukuaji na kuongeza thamani ya muda mrefu kwa wanahisa wetu.

## Hitimisho

Namalizia kwa kutoa shukrani za dhati kwa wafanyakazi wetu na timu yetu ya uongozi wa benki katika ngazi mbali mbali kwa mchango wao mkubwa katika kutekeleza malengo ya benki yetu, Bodi ya Wakurugenzi kwa mwongozo wao, wasimamizi wetu kwa usaidizi wao wa karibu, na kwa wanahisa na wateja wetu kwa uaminifu na msaada wao usio na kifani.



**RESPIGE KIMATI**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**26 JULAI 2025**

# DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA TANO

## AJENDA YA 3

**KUTHIBITISHA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANAHISA WA 15 ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MARANTA, MSIMBAZI CENTRE JIJINI DAR ES SALAAM JULAI 27, 2024**

## WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Gasper Njuu | - | Mwenyekiti |
| 2. | Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | - | Mjumbe |
| 3. | Bw. Benedict Sudi | - | Mjumbe |
| 4. | Bw. Martin Mdoe | - | Mjumbe |
| 5. | Bi. Uphoo Swai | - | Mjumbe |
| 6. | Bw. Robert Mtendamema | - | Mjumbe |
| 7. | Bw. Respige Kimati | - | Mkurugenzi Mtendaji |
| 8. | Bi. Paulina Kunjumu | - | Katibu wa Kampuni |

## WAJUMBE WA BODI WALIOTOA UDHURU

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Padre Dkt. Charles Kitima | - | Mjumbe |

## WAGENI WAALIKWA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Cletus Kiyuga | - | Mwakilishi wa PwC |
| 2. | Bi. Jesca Thobias Jenge | - | Mwakilishi wa Mamlaka ya Mitaji na Masoko ya Dhamana (CMSA) |
| 3. | Bi. Mariam Omari Mtunguja | - | Mwakilishi wa Mamlaka ya Mitaji na Masoko ya Dhamana (CMSA) |

## WANAHISA

| NA | JINA | HALI YAKE |
|---|---|---|
| 1 | ABEL BERA SEBASTIAN | Anatambulika |
| 2 | ABEL E. KUSIGA | Anatambulika |
| 3 | ABRAHAM A. MALEKO | Anatambulika |
| 4 | ABROGAST CHAMI | Anatambulika |
| 5 | ADELAIDA R. ASEY | Anatambulika |
| 6 | ADELINA DEOGRATIUS NJUNWA | Anatambulika |
| 7 | ADOULLAH THOMAS KOKO | Anatambulika |
| 8 | ADRIAN J. MAKELELE | Anatambulika |
| 9 | ADRIANO GERALD | Anatambulika |
| 10 | ADVENTINA KAILEMBO MULOKOZI | Anatambulika |
| 11 | AGATHA E. MAYEMBA | Anatambulika |
| 12 | AGNES MOSHA | Anatambulika |
| 13 | AGNESS ATHANA KISSUM | Anatambulika |
| 14 | AGNESS JOHN KIWIA | Anatambulika |
| 15 | AGRIPINA IBNASS MKAMY | Anatambulika |
| 16 | ALBANI PETER MWALO | Anatambulika |
| 17 | ALEX ATANAS | Anatambulika |
| 18 | ALEX NTANGULIGWA | Anatambulika |
| 19 | ALEX SIMON NGAIZA | Anatambulika |
| 20 | ALEX STEFANO KASILO | Anatambulika |
| 21 | ALFRED CHAMA MATIKO | Anatambulika |
| 22 | AMBROSE R. LYIMO | Anatambulika |
| 23 | ANANIAS K. WIGIRA | Anatambulika |
| 24 | ANASTAS LILONDO NGUNGURU | Anatambulika |
| 25 | ANASTASIA D. MASHURANO | Anatambulika |
| 26 | ANASTASIA MARO MTUMBUKA | Anatambulika |
| 27 | ANCILLA PESHA KASIMBAZI | Anatambulika |
| 28 | ANDREA M. MGAYA | Anatambulika |
| 29 | ANDREW EDWARD SALUMU | Anatambulika |
| 30 | ANGELA J. KYAKULA | Anatambulika |
| 31 | ANGERA CHIWAYA | Anatambulika |
| 32 | ANJILA H. KASIMBA | Anatambulika |
| 33 | ANNA A. MVUNGI | Anatambulika |
| 34 | ANNA F. SHAO | Anatambulika |
| 35 | ANNA WANGAEL SWAI | Anatambulika |
| 36 | ANSILA BENO JOHN | Anatambulika |
| 37 | ANTHONY JAMES LUBUVA | Anatambulika |
| 38 | ANUCIATHA KAWISHA | Anatambulika |
| 39 | ANZIGAR ROBERT MAPUNDA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 40 | APOLINARY B.MWARABU | Anatambulika |
| 41 | ARBOCAST ST. NDUBA KUZENZA | Anatambulika |
| 42 | ARCHDIOCESE OF MWANZA | Anatambulika |
| 43 | ARNOLD MSENGEZI | Anatambulika |
| 44 | ASUNTA V. IKUNKO | Anatambulika |
| 45 | AUDAX JOSEPHAT RUTA | Anatambulika |
| 46 | AUGUSTINE PAULO MSETI | Anatambulika |
| 47 | AUGUSTINE R. KASHULI | Anatambulika |
| 48 | AVELINA L. HOKORORO | Anatambulika |
| 49 | BABINA BALTAZARY SHAYO | Anatambulika |
| 50 | BALTAZAR I. MASSAWE | Anatambulika |
| 51 | BALTAZAR W. MWEIRO | Anatambulika |
| 52 | BEATRICE AGUST MTEY | Anatambulika |
| 53 | BEATRICE KAHOHO | Anatambulika |
| 54 | BEATRICE KAMPUGA | Anatambulika |
| 55 | BENNET CHARLES MAULAH | Anatambulika |
| 56 | BERNADETA KATANDALILA | Anatambulika |
| 57 | BERTOLD NJAWIKE | Anatambulika |
| 58 | BETWIAL BEATUS MANYAKU | Anatambulika |
| 59 | BIBIANA NGOWI | Anatambulika |
| 60 | BIKIRA MARIA SALASALA | Anatambulika |
| 61 | BISMASS ISSA MLUNGAMO | Anatambulika |
| 62 | BONITUS DOMINIC MWALLENI | Anatambulika |
| 63 | BUGANDO MEDICAL CENTRE | Anatambulika |
| 64 | CALISTUS PHILIP ASSENGA | Anatambulika |
| 65 | CAMILLIAN FAMILY | Anatambulika |
| 66 | CATHERINE C. MNGANYA | Anatambulika |
| 67 | CATHERINE MWIDETE | Anatambulika |
| 68 | CATHERINE VINGILLAH | Anatambulika |
| 69 | CHARLES M. LUSAYA | Anatambulika |
| 70 | CHARLES RUGARABAMU | Anatambulika |
| 71 | CHRISTA FRANCIS CHILALA | Anatambulika |
| 72 | CHRISTINA FABIAN KAPEMBE | Anatambulika |
| 73 | CHRISTINA MATERU | Anatambulika |
| 74 | CHRISTOPHER V. MTALIMWA | Anatambulika |
| 75 | CLEMENT KIDALA | Anatambulika |
| 76 | CLEOPHAS G. MWANGONELA | Anatambulika |
| 77 | CLEOTILDA W. MAKAVA | Anatambulika |
| 78 | CLEVINA TIBAMANYA | Anatambulika |
| 79 | CONSOLATA ALBERT BEBWA | Anatambulika |
| 80 | CONSTINE DANIEL MSIKE | Anatambulika |
| 81 | COSTANTINE C. MSHANGA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 82 | COSTANTINE MALIGANYA NG'HWENGE | Anatambulika |
| 83 | CUTHBERT KARLIHANGA | Anatambulika |
| 84 | CYPRIAN KRISPIN | Anatambulika |
| 85 | DAMIAN ELIAS MREMA | Anatambulika |
| 86 | DANIEL J. KULULYA | Anatambulika |
| 87 | DANIEL M. UBALANJE | Anatambulika |
| 88 | DANIEL MEHAN KINDAGARTEN | Anatambulika |
| 89 | DANIEL MLEMETA MWENDI | Anatambulika |
| 90 | DANIEL P.NDANGA | Anatambulika |
| 91 | DANIELA JOSEPH MWINUKA | Anatambulika |
| 92 | DANSTAN INYASI MASSAWE | Anatambulika |
| 93 | DAUD J. PANGILA | Anatambulika |
| 94 | DAVINA P. MATOLA | Anatambulika |
| 95 | DEOGRATIAS KAMUGISHA | Anatambulika |
| 96 | DEOGRATIUS | Anatambulika |
| 97 | DESIDERATO ATILIO MKEMWA | Anatambulika |
| 98 | DESIDERI J. MULAGALA | Anatambulika |
| 99 | DESIDERY KAKWEZI ATHANAS | Anatambulika |
| 100 | DEVOTHA B. GERALDI | Anatambulika |
| 101 | DINA HAITA MBUBA | Anatambulika |
| 102 | DINA S. MASENGA | Anatambulika |
| 103 | DIOCRES G. RUTAZA | Anatambulika |
| 104 | DISMASIA E. LYANGANI | Anatambulika |
| 105 | DOMINIC B. MASSAWE | Anatambulika |
| 106 | DONADONI ATILIO MKEMWA | Anatambulika |
| 107 | DONATI PASKALI | Anatambulika |
| 108 | DORAH MWITA | Anatambulika |
| 109 | DORIS EDWARD NYATAHE | Anatambulika |
| 110 | DR. KEBRON MAHOO | Anatambulika |
| 111 | DR. ROSE BENEDICT OLOMI | Anatambulika |
| 112 | DR. WOLAEGHIORGHIS VILLA | Anatambulika |
| 113 | EDMUND E. MUNISHI | Anatambulika |
| 114 | EDMUND HENRY KAGIMBO | Anatambulika |
| 115 | EDWALD N. MREMA | Anatambulika |
| 116 | EDWARD STAMBULY | Anatambulika |
| 117 | EDWIN ALIKO SAIJENI | Anatambulika |
| 118 | EDWIN P. MUNGA | Anatambulika |
| 119 | EDWINA A. LUPEMBE | Anatambulika |
| 120 | ELEONORA MATHIAS MROSSO | Anatambulika |
| 121 | ELIAS A. MMARI | Anatambulika |
| 122 | ELIZABETH BONIPHAS | Anatambulika |
| 123 | ELIZABETH FRANK FOVO | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 124 | ELIZABETH IGNACE MOWO | Anatambulika |
| 125 | ELIZABETH M. MASOI | Anatambulika |
| 126 | ELIZABETH PANCRASS TAIRO | Anatambulika |
| 127 | ELIZABETH STUWAT MBAGO | Anatambulika |
| 128 | EMELDA CHARLES MWENDA | Anatambulika |
| 129 | EMERENCIANA L.UTOUH | Anatambulika |
| 130 | EMILIANA G. TABAILLE | Anatambulika |
| 131 | EMILIANA MASOUD MIASY | Anatambulika |
| 132 | EMMANUEL ANTHONY KULANGESIWA | Anatambulika |
| 133 | EMMANUEL J. BUKANGO | Anatambulika |
| 134 | EMMANUEL JJ BUKANGO | Anatambulika |
| 135 | EMMY M. MAGENI | Anatambulika |
| 136 | ENATA NONGA | Anatambulika |
| 137 | ENOCK F.KIKOTI | Anatambulika |
| 138 | ERIC A. K. MARENGE | Anatambulika |
| 139 | ERICK F. LUBUSA | Anatambulika |
| 140 | ERICK MWARABU | Anatambulika |
| 141 | ESTHER BUKANGO | Anatambulika |
| 142 | EUTROPEA H. MARO | Anatambulika |
| 143 | EVELYN XAVIER KAYOMBO | Anatambulika |
| 144 | EXPEDITO DICKENS SIMMON | Anatambulika |
| 145 | EZEKIEL FELIX ISSAKA | Anatambulika |
| 146 | FAUSTUS GWIMO RUGONDA | Anatambulika |
| 147 | FEBROSIA H. KAPINGA | Anatambulika |
| 148 | FELISTER N. MPEMBA | Anatambulika |
| 149 | FLORA MBIGWA | Anatambulika |
| 150 | FLORENTS M. SEIYA | Anatambulika |
| 151 | FORTUNATA ALLI MEHARAZO | Anatambulika |
| 152 | FR ENGLBERT NYANDWI | Anatambulika |
| 153 | FR FRASTO NAAKULE | Anatambulika |
| 154 | FR SELESTINE KAPINGA | Anatambulika |
| 155 | FRED HABIBU KATAWAA | Anatambulika |
| 156 | FROLIAN DEOGRATIAS MUTASIGWA | Anatambulika |
| 157 | GANDOLF C. ASENGA | Anatambulika |
| 158 | GASPER O. MBILINYI | Anatambulika |
| 159 | GAUDENSIA CALIST | Anatambulika |
| 160 | GENEROSA JOSEPH RUTAIHWA | Anatambulika |
| 161 | GEOFREY F. MROSO | Anatambulika |
| 162 | GEORGE SALESIAN LUKOA | Anatambulika |
| 163 | GERALD A. MKOBA | Anatambulika |
| 164 | GERMANA G. MABUNGA ITF BRENDA NYAMIZI MNARO | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 165 | GERVAS JOSEPH KAVISHE | Anatambulika |
| 166 | GERVAS LAZARO MBILINYI | Anatambulika |
| 167 | GETRUDE C. NGUBIAGAI | Anatambulika |
| 168 | GIBSON AKIM | Anatambulika |
| 169 | GODFRIDA M. TESHA | Anatambulika |
| 170 | GODLIVER M. RWEYEMAMU | Anatambulika |
| 171 | GODWIN THOBIAS MWITA | Anatambulika |
| 172 | GRACE A. MUSHY | Anatambulika |
| 173 | GRACE BEDA MINJA | Anatambulika |
| 174 | HAPPINESS M. | Anatambulika |
| 175 | HAPPY SAIMON MJEMA | Anatambulika |
| 176 | HARRY D. CHOPETA | Anatambulika |
| 177 | HENRY JOSEPH MBOYA | Anatambulika |
| 178 | HENRY MWOLEKA MUTEMBEI | Anatambulika |
| 179 | HERMENILDEY NGUMBE | Anatambulika |
| 180 | HERMOGEN B. NGOTEZI | Anatambulika |
| 181 | HILDA FLORENCE KASONSO | Anatambulika |
| 182 | HUGO E. SHIRIMA | Anatambulika |
| 183 | HUSNA HAJI KAVISHE | Anatambulika |
| 184 | IBRAHIM K. MGETA | Anatambulika |
| 185 | IGNACE MARINGA PETER MOWO | Anatambulika |
| 186 | IMAKULATA GHAFUMBWE | Anatambulika |
| 187 | IMMACULATA D. MUTASHAIRWA | Anatambulika |
| 188 | INNOCENT D. ALEX | Anatambulika |
| 189 | INNOCENT M. KAPALALE | Anatambulika |
| 190 | IRMINA MBULA MILLANZA | Anatambulika |
| 191 | JACKSON MSOKA | Anatambulika |
| 192 | JACOB BWANATUMBO | Anatambulika |
| 193 | JAMES KIWALI MALLYA | Anatambulika |
| 194 | JAMES M. BENEDICT | Anatambulika |
| 195 | JANE JAPHET MALLYA | Anatambulika |
| 196 | JANEMARY RUTAHOILE | Anatambulika |
| 197 | JANETH JOSEPH MKOMBACHEPA | Anatambulika |
| 198 | JANUARY M. MSHIMBO | Anatambulika |
| 199 | JASTAS S. MKONGORO | Anatambulika |
| 200 | JESCA JENGE | Anatambulika |
| 201 | JESCA JOEL KABALINALI | Anatambulika |
| 202 | JIMBO CATHOLIC MOSHI | Anatambulika |
| 203 | JNNK MT. LUCIA KRISTO MFALME | Anatambulika |
| 204 | JOAN JASTIN KAUSHE | Anatambulika |
| 205 | JOHN EWALD MOSHY | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 206 | JOHN GASPER SIMBEYA | Anatambulika |
| 207 | JOHN INYASI MASSAWE | Anatambulika |
| 208 | JOHN J. KILLIWA | Anatambulika |
| 209 | JOHN KIIZA | Anatambulika |
| 210 | JOHN MDENDE BIZONGWAKO | Anatambulika |
| 211 | JOHN MG GROUP | Anatambulika |
| 212 | JOHN RAPHAEL KIMATA | Anatambulika |
| 213 | JOSEPH JAMES KESSY | Anatambulika |
| 214 | JOSEPH JAPHET SAMILE | Anatambulika |
| 215 | JOSEPH S. MREMA | Anatambulika |
| 216 | JOSEPH YOSEYA KASYANJO | Anatambulika |
| 217 | JOSEPHAT P. MBILINYI | Anatambulika |
| 218 | JOSEPHINA JOHN MAZOMPOLO | Anatambulika |
| 219 | JUDITH R. MKOBA | Anatambulika |
| 220 | JULIETH GODFREY LUSUILWA | Anatambulika |
| 221 | JULIUS B. MBAWALA | Anatambulika |
| 222 | JUMANA JOSEPH ANDREA | Anatambulika |
| 223 | JUMANNE S. SELEMANI | Anatambulika |
| 224 | JUMUIYA MT. PADRE PIO | Anatambulika |
| 225 | JUMUIYA YA MT. CESILIA | Anatambulika |
| 226 | JUMUIYA YA MT. MONICA | Anatambulika |
| 227 | KARISTO A. MFALAMAGOHA | Anatambulika |
| 228 | KARSMATIKI KATOLIKI YOMBO | Anatambulika |
| 229 | KISCIMBO NARZIS | Anatambulika |
| 230 | KOLETHA MWALUGENGE | Anatambulika |
| 231 | KUMBUKA E. MANOZA | Anatambulika |
| 232 | KWAYA YA UPENDO | Anatambulika |
| 233 | LAMBERTHA HYASINT MAHAI | Anatambulika |
| 234 | LAURENT M. MAYOLI | Anatambulika |
| 235 | LEOCADIA RUOTI MKOJI | Anatambulika |
| 236 | LEONARDINA I. MAPUNDA | Anatambulika |
| 237 | LEONCE GILLETTE LYIMO | Anatambulika |
| 238 | LETICIA M.CHAMBILA | Anatambulika |
| 239 | LEVINA CHRISTOPHER MTALEMWA | Anatambulika |
| 240 | LEVINA MICHAEL MOMBURI | Anatambulika |
| 241 | LIDWINI THOMAS LUVANDA | Anatambulika |
| 242 | LIGHTNESS CASTORY MBUTA | Anatambulika |
| 243 | LUCASA. MAGALI | Anatambulika |
| 244 | LUCIANA ADRIAN MADUGA | Anatambulika |
| 245 | LUCY GEORGE MAYAO | Anatambulika |
| 246 | LUDWINA A. MLAY | Anatambulika |
| 247 | LUSIMA KURINGE MSOMA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 248 | LUTIGARA LUCAS RWEZAULA | Anatambulika |
| 249 | MARCO JUSTINE MWENDA | Anatambulika |
| 250 | MARGAARETH P. JOHN | Anatambulika |
| 251 | MARTIN MATEI KIMATH | Anatambulika |
| 252 | MARTIN R. SIWINGWA | Anatambulika |
| 253 | MARY K. TEMBA | Anatambulika |
| 254 | MARY LUCAS | Anatambulika |
| 255 | MARY MAHOCHO MSEMWA | Anatambulika |
| 256 | MARY MCHOME | Anatambulika |
| 257 | MARY V. URASSA | Anatambulika |
| 258 | MARYGOLET ARIKADI RWIZA | Anatambulika |
| 259 | MATHEW J. KAZEZE | Anatambulika |
| 260 | MATHIAS C. MKULA | Anatambulika |
| 261 | MATHIAS KWABI SHIMIJI | Anatambulika |
| 262 | MATHIAS L. LAURENT | Anatambulika |
| 263 | MATHIAS MUJUAMUNGU | Anatambulika |
| 264 | MAURA STEPHEN MBENNA | Anatambulika |
| 265 | MAXIMUS BUHAGIZI | Anatambulika |
| 266 | MAY H.MUNGILWA | Anatambulika |
| 267 | MCODEMA THOMAS | Anatambulika |
| 268 | MECKIADES MSIMBE | Anatambulika |
| 269 | MECTIDIS C. | Anatambulika |
| 270 | MELANIA ICHAEL MAGESA | Anatambulika |
| 271 | MESHACK CHACHA MANGENGI | Anatambulika |
| 272 | METHOD LUDOVICK | Anatambulika |
| 273 | MICHAEL S. URIO | Anatambulika |
| 274 | MICHAEL YEREMIA LUVANGA | Anatambulika |
| 275 | MODESTA M LENGO | Anatambulika |
| 276 | MODESTA P. MWALO | Anatambulika |
| 277 | MOHAMED SALIMU MHARIZO | Anatambulika |
| 278 | MOYO MT WA YESU | Anatambulika |
| 279 | MSIMBAZI PARISH | Anatambulika |
| 280 | MT YOHANA BATIZAJI KIWALANI YOMBO | Anatambulika |
| 281 | NAIMI S. MASSAWE | Anatambulika |
| 282 | NATALIA H. SHIRIMA | Anatambulika |
| 283 | NAZARIUS P. CHONYA | Anatambulika |
| 284 | NEEMA M. NUNGU | Anatambulika |
| 285 | NEMES T. MKUDE | Anatambulika |
| 286 | NICODEMOS J. KISHEO | Anatambulika |
| 287 | OCTAVIAN MSOFU | Anatambulika |
| 288 | OLIVER ANTHONY KULANGISIWA | Anatambulika |
| 289 | OLYMPIA ODILLO | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 290 | ONESMO RICHARD NDAKI | Anatambulika |
| 291 | OSCAR M. MAWSHA | Anatambulika |
| 292 | PASCHAL MALIFEDHA KANYALA | Anatambulika |
| 293 | PASSIAN J. MATHIAS | Anatambulika |
| 294 | PASTORY KATUNZI RWEGOSHORA | Anatambulika |
| 295 | PASTORY M.MSANYA | Anatambulika |
| 296 | PATRICIA F. MWANUKUZI | Anatambulika |
| 297 | PATRICK NDERINA SHIRIMA | Anatambulika |
| 298 | PAUL KALINJUMA DAUDI | Anatambulika |
| 399 | PAUL LIWAGI MULINGA | Anatambulika |
| 300 | PAUL S. SHEMWETA | Anatambulika |
| 301 | PAULINA P. NYAKI | Anatambulika |
| 302 | PELAGIA STEPHANO NYONI | Anatambulika |
| 303 | PERAGIA KAWAMALA CHARLES | Anatambulika |
| 304 | PERAMIHO MAJOR SEMINARY | Anatambulika |
| 305 | PERPETUA E. ISHABAKAKI | Anatambulika |
| 306 | PETER JAMES KESSY | Anatambulika |
| 307 | PETER MWITA NYANOKWE | Anatambulika |
| 308 | PHILIP LAWRENCE MJEMA | Anatambulika |
| 309 | PHILOMENA LEONARD LYARUU | Anatambulika |
| 310 | PIUS GABRIEL SIRIWA | Anatambulika |
| 311 | PRAXEDY VINCENT CHACKY | Anatambulika |
| 312 | PRIMITIVA P. RAMUGISHA | Anatambulika |
| 313 | PROGENETHA K. IBRESK | Anatambulika |
| 314 | PROSPER E. ULOTU | Anatambulika |
| 315 | PUCKERIA EMILI | Anatambulika |
| 316 | RAPHAEL E. MROSSO | Anatambulika |
| 317 | RASHID A. KUPYASA | Anatambulika |
| 318 | RAY E. KIMBITON | Anatambulika |
| 319 | RAYMOND KURINGE MSOMA | Anatambulika |
| 320 | RAYNALDA FIDELIS NGOMBALE | Anatambulika |
| 321 | RDT EDW ARD A MWESIUMO | Anatambulika |
| 322 | REGINA A. HINGA | Anatambulika |
| 323 | REGINA JOEL KABALIBALI | Anatambulika |
| 324 | REGINA MGULA | Anatambulika |
| 325 | RENATUS R. MWAKIMBWALA | Anatambulika |
| 326 | REUBENI P. MMAJO | Anatambulika |
| 327 | REVOCATUS R. MSHEMA | Anatambulika |
| 328 | REVOCATUS SANKA & FAMILY | Anatambulika |
| 329 | RHODA A. D. KWEKA | Anatambulika |
| 330 | RICHARD B. KABYENDA | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 331 | RICHARD M MAHUNDI | Anatambulika |
| 332 | RICHARD M. KAYOMBO | Anatambulika |
| 333 | RICHARD PHILLIP MBOGO | Anatambulika |
| 334 | ROMANA V. MILLEMBE | Anatambulika |
| 335 | ROSADA SHAO | Anatambulika |
| 336 | ROSALIA D. WATUGULU | Anatambulika |
| 337 | ROSALIA KOMBA | Anatambulika |
| 338 | ROSE BONITO MBUTA | Anatambulika |
| 339 | ROSE FRANCIS MAIGE | Anatambulika |
| 340 | ROSE JOHN KIYEYEU | Anatambulika |
| 341 | ROSE KIPAMI MWENZEGULE | Anatambulika |
| 342 | ROZALDINA H. MANJWA | Anatambulika |
| 343 | RUAHA CATHOLIC UNIVERSITY(RUCO) | Anatambulika |
| 344 | RUDOLF ATILIO MKEMWA | Anatambulika |
| 345 | RUSTUS ALOIS | Anatambulika |
| 346 | SABAZ T. MWISHO | Anatambulika |
| 347 | SABINA GABRIEL MOSHY | Anatambulika |
| 348 | SABINA M. LUJUA | Anatambulika |
| 349 | SAIDAN R. MBIRO | Anatambulika |
| 350 | SALOME C. MAKAMBI | Anatambulika |
| 351 | SALUSTIAN T. NKOLA | Anatambulika |
| 352 | SALVATORIAN SISTERS | Anatambulika |
| 353 | SALVATORIAN SISTERS ITF MEHAN | Anatambulika |
| 354 | SALVATORIAN SISTERS OF THE DIVINE | Anatambulika |
| 355 | SALVATORY MUSHI | Anatambulika |
| 356 | SC. PASCOLINA LOWE OSBCAM | Anatambulika |
| 357 | SCHOLASTICA JOHN NTIRUKA | Anatambulika |
| 358 | SEBASTIAN SAMBUO MUSHI | Anatambulika |
| 359 | SECELELA J. HOKORORO | Anatambulika |
| 360 | SELESTIN W. DIDAS | Anatambulika |
| 361 | SELINA DAUD MREFU KUBOJA | Anatambulika |
| 362 | SELINA MLIMGI | Anatambulika |
| 363 | SEVERINI K. NYEHO | Anatambulika |
| 364 | SHEDRACK M. KISINGA | Anatambulika |
| 365 | SIMON M. MAPALALA | Anatambulika |
| 366 | SIMON P. MRINA | Anatambulika |
| 367 | SOPHIA G. MWAKILASA | Anatambulika |
| 368 | SR MECTIDLES NGURUWE OSBCAM | Anatambulika |
| 369 | SR. CATHERINE NJIRU | Anatambulika |
| 370 | SR. FLORENCE MHAGAMA | Anatambulika |
| 371 | SR. MARCELLA MINDE | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 372 | ST. JOHN BOSCO PARISH | Anatambulika |
| 373 | STANSLAUS W. MTAMBWA | Anatambulika |
| 374 | STELLA CHARLES MIHAMBO | Anatambulika |
| 375 | STELLA P. BUNDALA | Anatambulika |
| 376 | SUZANNE STAMBULY | Anatambulika |
| 377 | SUZO H. KAZIMOTO | Anatambulika |
| 378 | TAUSI ROBERT KWIMBA | Anatambulika |
| 379 | TEDY ANDREW SALUMU | Anatambulika |
| 380 | TEOTIM RICHADI MMANDA | Anatambulika |
| 381 | TANZANIA EPISCOPAL CONFERENCE | Anatambulika |
| 382 | THADEO PIUS KABUNDUGULU | Anatambulika |
| 383 | THECIA I. MALLINDI | Anatambulika |
| 384 | THEODORA SABIUS MAKAUSHE | Anatambulika |
| 385 | THEODOSIA THOMAS CHUWA | Anatambulika |
| 386 | THEOPISTA STEPHEN TARIMO | Anatambulika |
| 387 | THERESIA EPAFRA KESSY | Anatambulika |
| 388 | THERESIA MALATA SHIYO | Anatambulika |
| 389 | THERESIA O. MSANGIRA | Anatambulika |
| 390 | THERESIA ZAWADI NKUJA | Anatambulika |
| 391 | THOMAS J. NGWALA | Anatambulika |
| 392 | UFUMWA SACCOS | Anatambulika |
| 393 | USHIRIKA WA NGONYAMA | Anatambulika |
| 394 | UTOTO MTAKATIFU MSIMBAZI | Anatambulika |
| 395 | VALENCE A. KATUMWA | Anatambulika |
| 396 | VALERIANA MT. IGNAS YOMBO | Anatambulika |
| 397 | VENERANDA DYETA KAPERA | Anatambulika |
| 398 | VERDIANA MASSINDE MARGAI | Anatambulika |
| 499 | VERONICA L. | Anatambulika |
| 400 | VERONICA T. KIIZA | Anatambulika |
| 401 | VIANEY P. LINGA | Anatambulika |
| 402 | VICKY M. LAFFA | Anatambulika |
| 403 | VICTORIA ALPHONCE GANAI | Anatambulika |
| 404 | VICTORIA C. LUKWEMBA | Anatambulika |
| 405 | VICTORIA E. LUKUMBA | Anatambulika |
| 406 | VICTORIA HUGO SHIRIMA | Anatambulika |
| 407 | VICTORIA KIHWILI | Anatambulika |
| 408 | VIRGINIA VUMILIA | Anatambulika |
| 409 | WAJANE KIMARA | Anatambulika |
| 410 | WAKILI S. ALAWI | Anatambulika |
| 411 | WAWATA PAROKIA MICHUNGWANI | Anatambulika |
| 412 | WAWATA ST. JOSEPH | Anatambulika |

| | | |
|---|---|---|
| 413 | WAZO MOJA ASSOCIATION | Anatambulika |
| 414 | WINIFRIDA KAMUGISHA | Anatambulika |
| 415 | YAVAN SHEDRACK FOYA | Anatambulika |
| 416 | YOLATHA BAZIL | Anatambulika |
| 417 | YOSEPH GODFREY TARIMO | Anatambulika |
| 418 | YULANA METHOD KAMUGISHA | Anatambulika |
| 419 | ZACHARIA ANDREA MAHAJILE | Anatambulika |
| 420 | ZERNO THOMASIOSISY LUKWEMBA | Anatambulika |

## 1.0 KUFUNGULIWA KWA MKUTANO

Mwenyekiti aliitisha mkutano saa 10:15 asubuhi.

## 2.0 KUPITISHWA KWA AJENDA

Ajenda zifuatazo zilipitishwa:

2.1 Kufungua Mkutano;

2.2 Kupitishwa kwa ajenda;

2.3 Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Nne uliofanyika tarehe 29 Julai 2023;

2.4 Kupokea na kujadili mambo yanayotokana na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kumi na Nne uliofanyika tarehe 29 Julai 2023;

2.5 Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa ya Wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2023;

2.6 Kupokea, kujadili na kuidhinisha taarifa za kifedha za Benki pamoja na taarifa ya mkaguzi wa nje kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2023;

2.7 Kuteua mkaguzi wa hesabu wa nje;

2.8 Kupendekeza tarehe ya kufanyika kwa Mkutano Mkuu ujao;

2.9 Mengineyo; na

2.10 Kufungwa Mkutano.

## 3.0 UTHIBITISHO WA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA NNE ULIOFANYIKA TAREHE 29 JULAI, 2023.

3.1 Wanahisa walithibitisha kuwa kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne wa Mwaka uliofanyika tarehe 29 Julai, 2023 zilizowasilishwa zilikua sahihi.

## 4.0 KUPOKEA NA KUJADILI MAMBO YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA NNE ULIOFANYIKA TAREHE 29 JULAI, 2023.

4.1 ILIRIPOTIWA kuwa agizo la Wanahisa la kuboresha chapa ya vifaa vya Mkutano Mkuu wa Mwaka kwa kutoandika mwaka wa mkutano kwenye vifaa hivyo limeanza kutekelezwa na litaendelea kuzingatiwa kwenye mikutano ijayo. Bodi ya Wakurugenzi ilihakikisha kuwa vifaa vya Mkutano Mkuu wa 15 havikuwekwa mwaka wa mkutano, ili viweze kutumika tena katika shughuli za kila siku kama namna moja ya kutangaza huduma za benki.

4.2 ILIRIPOTIWA kuwa agizo la kuhakikisha vifaa vya Mkutano Mkuu wa Mwaka vinatofautiana na siyo fulana pekee limetekelezwa. Bodi ya Wakurugenzi ilihakikisha kuwa katika Mkutano Mkuu wa 15, Wanahisa walipatiwa vifaa mbalimbali vya kushiriki katika mkutano vikiwemo mabegi, daftari, kalamu, pamoja na fulana na vitenge.

4.3 ILIRIPOTIWA kuwa agizo la kuboresha utendaji wa benki na utekelezaji wa miradi ili benki iweze kulipa gawio kwenye Mkutano Mkuu ujao linaendelea kutekelezwa. Mwaka 2023, benki ilipata mafanikio makubwa kwenye viashiria muhimu vya kifedha kwa mfano Uwiano wa Gharama kwa Mapato (CIR) ulikua 62% sawa na mwaka 2022. Uwiano wa Mikopo chechefu (NPL) ulishuka hadi 8% kutoka 9%, Mapato kutokana na Mtaji (ROE) yalipanda hadi 25% kutoka 20%, Mapato kutokana na Mali (ROA) yaliongezeka hadi 3% kutoka 2%. Mafanikio haya yanaimarisha uwezo wa kifedha wa benki na yanaongeza uwezekano wa benki kulipa gawio mwaka 2025.

4.4 ILIRIPOTIWA kuwa agizo la kuongeza upatikanaji wa huduma za benki kwenye makanisa na taasisi zake limeendelea kutekelezwa. Tangu Mkutano Mkuu uliopita, benki ilianzisha vituo 12 vya Mkombozi Wakala vinavyoendeshwa kupitia Parokia. Mwaka 2024, benki ilibadilisha mfumo wa usimamizi wa wakala hao kwa kushirikiana na Parokia kwa kuongeza chapa ya kuvutia na kutenga watu maalum wa mauzo. Kupitia mfumo huu mpya, benki inalenga kufungua vituo vipya 60 vya Mkombozi Wakala ifikapo 31 Desemba 2024.

4.5 ILIRIPOTIWA kuwa agizo la kutangaza bidhaa na huduma za benki kwa kutumia makundi maalum kama wanawake, vijana na watoto limetekelezwa. Benki inaendelea kutumia majukwaa mbalimbali kufikisha ujumbe wake ikiwa ni pamoja na mitandao ya kijamii (Twitter, Facebook, Instagram, tovuti ya benki), pamoja na mitandao ya makanisa kama Tumaini Media, Tumaini TV, magazeti ya Kiongozi, Tumaini Letu, na majukwaa mengine ndani ya Kanisa ili kuongeza uelewa kuhusu huduma zake.

## 5.0 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2023.

5.1 ILIRIPOTIWA kuwa benki iliendelea kutoa huduma za kibenki na huduma zinazohusiana kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006, na kwamba hakukuwa na mabadiliko yoyote katika majukumu ya msingi ya benki kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023.

5.2 ILIRIPOTIWA kuwa jumla ya hisa 23,555,002 zilikua zimelipiwa mwishoni mwa mwaka 2023.

5.3 ILIRIPOTIWA kuwa jumla ya Wakurugenzi wanane (8), akiwemo Mkurugenzi Mtendaji, walihudumu kwenye Bodi ya Wakurugenzi wa benki katika kipindi hicho, na hakuna mkurugenzi aliyemiliki zaidi ya asilimia 0.3 ya jumla ya mtaji wa hisa za benki uliotolewa.

5.4 ILIRIPOTIWA kuwa Bodi ya Wakurugenzi iliendelea kuwajibika katika kuhakikisha kwamba taratibu na kanuni zote za uendeshaji wa benki zinafuatwa. Vilevile, shughuli za kila siku za benki zilisimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji akisaidiwa na timu ya menejimenti.

5.5 ILIRIPOTIWA kuwa benki ilipata faida kabla ya kodi (PBT) ya TZS milioni 8,572 kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2023 (2022: TZS milioni 5,145). Viashiria vingine vya utendaji vilikuwa kama ifuatavyo:

5.5.1 Mapato halisi ya uendeshaji yalifikia TZS milioni 25,226 ikilinganishwa na TZS milioni 21,097 mwaka 2022, hasa kutokana na kuongezeka kwa mapato yasiyotokana na riba kwa TZS milioni 3,407 (asilimia 60).

5.5.2 Amana za wateja ziliongezeka hadi TZS milioni 207,397 kutoka TZS milioni 184,579 mwaka 2022. Ongezeko hilo la asilimia 12 lilitokana na mikakati ya uhamasishaji wa amana pamoja na maboresho ya miundombinu ya huduma za benki.

5.5.3 Jumla ya mali za benki ziliongezeka hadi TZS milioni 255,789 kutoka TZS milioni 221,722 mwaka 2022, hasa kutokana na ongezeko la TZS milioni 34,067 katika mikopo na mapato kwa wateja na benki nyingine.

5.5.4 Gharama za uendeshaji zilifikia TZS milioni 16,654 ikilinganishwa na TZS milioni 15,951 mwaka 2022. Ongezeko hilo dogo la asilimia 4 lilitokana na upanuzi wa biashara kupitia matawi mapya ya Arusha na Bugando.

5.5.5 Mikopo iliongezeka hadi TZS milioni 134,261 kutoka TZS milioni 115,039 mwaka 2022, ongezeko la asilimia 17 kutokana na maboresho katika mchakato wa utoaji mikopo na nafasi nzuri ya mitaji.

5.5.6 Ubora wa mikopo uliendelea kudumishwa kwa kiwango cha mikopo chechefu (NPL) kufikia asilimia 8.

5.6 ILIRIPOTIWA kuwa Bodi ya Wakurugenzi ilifanya tathmini ya uendelevu wa benki na kubaini kuwa benki ina uwezo wa kuendesha shughuli zake kwa kipindi kirefu.

5.7 ILIRIPOTIWA kuwa Bodi haikupendekeza gawio kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2023 kwa sababu benki haikutimiza viwango vya uwiano vinavyotakiwa na Benki Kuu ya Tanzania, pamoja na kuwa katika mchakato wa kuongeza mtaji wa biashara.

5.8 ILIRIPOTIWA kuwa benki ilikuwa na wafanyakazi wa kutosha na wenye uzoefu wa kutekeleza shughuli zake na kutimiza mpango wa biashara wa benki.

5.9 ILIRIPOTIWA kuwa benki haikutoa msaada wowote kwa vyama vya siasa na iliendelea kuwa na uhusiano mzuri na wadau wake wote, wakiwemo kamati za usimamizi wa benki.

5.10 ILIRIPOTIWA kuwa huduma za kidijitali za benki ziliendelea kupata mwitikio mkubwa mwaka huo. Huduma ya mawakala (Mkombozi WAKALA), mfumo wa usimamizi wa fedha za makanisa (SADAKA Digital), huduma za benki mtandao na simu zilipata mafanikio makubwa kwa matumizi ya wateja.

5.11 ILIRIPOTIWA kuwa benki ilikamilisha hatua za maandalizi kwa ajili ya kuingia kwenye mfumo wa Serikali wa Malipo (GePG) na ilikuwa inasubiri idhini kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuendelea na utekelezaji, ikitarajiwa kwamba utekelezaji huo utaanza robo ya pili ya mwaka 2024.

5.12 ILIRIPOTIWA kuwa benki ilitekeleza mfumo wa usimamizi wa fedha kwa shule (School Cash Management Solution), ambao ulikuwa katika hatua ya majaribio ya watumiaji (UAT), na ulipangwa kuzinduliwa robo ya pili ya 2024.

5.13 ILIRIPOTIWA kuwa benki ilikuwa katika maandalizi ya mfumo wa usimamizi wa fedha (Hospital Cash Management Solution) kwa hospitali, ambao umepangwa kuzinduliwa robo ya tatu ya 2024.

5.14 ILIRIPOTIWA kuwa benki ilikamilisha mipango na kufungua matawi mawili mapya Arusha na Mwanza (Bugando) mwezi Mei na Desemba 2023, ili kutimiza malengo ya mkakati wa kibiashara wa kuingia katika masoko mapya.

5.15 ILIRIPOTIWA kuwa benki ilikamilisha mpango wa kuhamishia Makao Makuu na tawi la St. Joseph katika jengo jipya la St. Joseph House mwezi Novemba 2023, ikiwa ni juhudi za kuboresha mazingira ya kazi na huduma kwa wateja.

5.16 ILIRIPOTIWA kuwa benki ilikuwa katika hatua za utekelezaji wa mfumo mpya wa Core Banking System, uliopangwa kukamilika mwisho wa mwaka 2024.

5.17 ILIRIPOTIWA kuwa juhudi za benki za kuimarisha biashara na kukuza mtaji zimeanza kuzaa matunda kupitia ongezeko la wateja, mapato, udhibiti wa gharama na usimamizi wa vihatarishi kwa ufanisi.

5.18 ILIRIPOTIWA kuwa Wanahisa waliipongeza Benki kwa mafanikio iliyoyapata katika mwaka 2023 na walitoa MAONI yafuatayo kutokana na majadiliano yaliyofanyika:

5.18.1 Kwamba kulikuwa na umuhimu wa kuboresha ufanisi wa uendeshaji wa huduma za uwakala wa benki ili wateja waweze kufikiwa na huduma katika maeneo ambayo Benki haina matawi. Benki iliripoti kuwa ilitekeleza mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma hizo, ikiwemo kuongeza idadi ya mawakala wakuu na kuwawezesha ili kuwasaidia mawakala wengine katika kanda husika, kuongeza usajili wa mawakala katika maeneo mbalimbali pamoja na kuwapatia vifaa na msaada unaohitajika kwa ajili ya kuhudumia wateja wa benki. Aidha, uandikishaji wa mawakala ulifanyika kwa watu wote, wale walio na uhusiano na kanisa na wale wasio na uhusiano na kanisa. Benki inaendelea na jitihada za kuboresha ufanisi wa mtandao wa mawakala katika kanda zote nchini ili kusogeza huduma kwa wateja wake.

5.18.2 Kwamba Benki ina idadi ndogo ya matawi katika kanda mbalimbali, hivyo kuna haja ya kuendeleza mikakati ya upanuzi kwa kuongeza matawi pamoja na utekelezaji wa njia mbadala za kutoa huduma kupitia mifumo ya kidijitali. Benki inaendelea na jitihada za kuhakikisha wateja wake wanapata huduma kupitia mifumo ya kidijitali na mtandao wa uwakala. Katika kipindi husika, Benki iliweza kufungua matawi kamili mawili katika maeneo ya Arusha na Mwanza ndani ya hospitali ya Bugando, na itaendelea na mpango wa kufungua matawi mengine kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Benki.

5.18.3 Kwamba kuna fursa nyingi za kibiashara katika maeneo kama Njombe, Kilombero na Ifakara ambazo Benki inapaswa kuzifanyia kazi. Wanahisa walishauri kuwa Benki iwe na uwepo katika maeneo hayo na maeneo mengineyo ili kuweza kupata wateja wapya na kutoa huduma na suluhisho za kifedha. Benki ilibainisha kuwa tayari ina matawi katika mkoa wa Njombe na Morogoro yanayohudumia mahitaji ya wateja wa maeneo hayo. Hata hivyo, Bodi iliahidi kuongeza juhudi za kuwafikia na kujihusisha zaidi na wateja katika maeneo hayo ili kunufaika na shughuli za kibiashara zilizopo.

5.18.4 Kwamba kuna taasisi nyingi za Kanisa ambazo hazitumii huduma za Benki kwa ajili ya malipo na miamala mbalimbali, badala yake zinatumia akaunti za benki nyingine. Wanahisa walitaka kufahamu mikakati iliyopo kuhakikisha taasisi hizo zinahamasishwa kutumia akaunti za benki. Bodi iliripoti kuwa mazungumzo na taasisi hizo yanaendelea ili kuwahamasisha kutumia akaunti

za Benki kwa ajili ya kufanya malipo na kuendesha shughuli mbalimbali za biashara na miradi.

5.18.5 Kwamba Benki haijalipa gawio kwa wanahisa katika miaka ya hivi karibuni. Benki ilieleza kuwa hali hiyo imetokana na malengo yake ya kukuza mtaji kwa ajili ya upanuzi pamoja na masharti ya kisheria yanayolazimisha Benki kufikia uwiano wa gharama na mapato (Cost to Income Ratio – CIR) wa 55% na kiwango cha mikopo chechefu (NPL ratio) kisichozidi 5% kama masharti ya kisheria kabla ya kulipa gawio.

5.18.6 Wanahisa walitaka kufahamu mikakati ya Benki kuhakikisha inazingatia na kufikia uwiano sahihi wa mikopo chechefu (NPL) na uwiano wa gharama kwa mapato (CIR) ili kuwezesha ulipaji wa gawio kwa miaka ijayo. Bodi ilieleza kuwa Benki imeweka mikakati ya kuboresha usimamizi wa mikopo ili kuzuia akaunti kuingia kwenye kundi la mikopo chechefu, huku ikihakikisha uwepo wa mikopo yenye ubora kwa kutoa mikopo mipya yenye viwango vya ubora. Aidha, Benki inaendelea na juhudi za kufufua akaunti chechefu ili ziweze kulipika na kurudisha faida kwa benki. Kuhusu uwiano wa gharama kwa mapato, Benki inaendelea na juhudi za kupunguza gharama za uendeshaji huku ikidumisha shughuli za upanuzi wa benki kwa kiwango kinachokubalika ili kufikia uwiano wa gharama kwa mapato unaokubalika.

5.18.7 Kwamba Benki inapaswa kuongeza matangazo ya bidhaa na huduma zake ili kupata wateja wengi na kuwa na nafasi kubwa katika soko. Bodi ilieleza kuwa Benki inaendelea kutumia majukwaa mbalimbali kufikisha taarifa za huduma zake na kuongeza uelewa wa bidhaa zake huku ikidumisha viwango bora vya huduma. Benki hutumia mitandao ya kijamii na mitandao ya Kanisa ili kuongeza uelewa kuhusu Benki na huduma zake.

5.18.8 Kwamba kuna wigo mpana wa wateja na fursa za kibiashara ndani ya Kanisa na taasisi zake zinazoweza kutumiwa na Benki. Bodi ilikubali hoja hiyo na kuahidi kuongeza ushirikiano na taasisi za Kanisa ili Benki iweze kushiriki katika miradi mbalimbali inayotarajiwa kutekelezwa, sambamba na kukuza amana na ukuaji wa Benki kwa ujumla.

5.18.9 Kwamba Benki inapaswa kuwa tayari na kuwa na uwezo wa kuwahudumia ipasavyo wateja wanaofika matawini kwa kuwapatia suluhisho za kifedha kwa weledi na kwa wakati. Bodi iliripoti kuwa Benki inaendelea na juhudi za kuboresha huduma kwa wateja wake katika matawi yake yote kwa kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa mafunzo ya kutoa huduma bora kwa wateja. Aidha, Benki inaboresha huduma kwa kufanya tathmini za mara kwa mara kuhusu

utendaji wa matawi na kushughulikia maoni na malalamiko yanayotolewa na wateja.

5.18.10 Kwamba Benki inapaswa kuhakikisha kuwa wanahisa wote wanapatiwa vitabu na nyaraka za Mkutano Mkuu kwa wakati kabla ya mkutano. Bodi ilikubali hoja hiyo na kuahidi kuwapatia vifaa wanahisa wote ambao hawakupokea baadhi ya vifaa hivyo, ikiwa ni pamoja na fulana na vitabu, baada ya mkutano. Wanahisa walielezwa kuwa nakala laini ya kitabu cha Mkutano Mkuu ilikuwepo kwenye tovuti ya benki na inaweza kupatikana wakati wowote. Bodi iliahidi kuhakikisha kuwa vifaa vya kutosha vya Mkutano Mkuu vinatolewa katika mikutano ijayo.

5.18.11 Kwamba Benki inapaswa kuzingatia uwezekano wa kuendesha mikutano ya mwaka ya wanahisa katika mikoa mingine badala ya Dar es Salaam pekee. Bodi ilipokea hoja hiyo kwa ajili ya kuifanyia kazi katika mipango ya mikutano ijayo.

5.18.12 Kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka unapaswa kuboreshwa kwa kuruhusu ushiriki wa wanahisa kupitia mtandao. Benki iliripoti kuwa mkutano wa aina mseto (hybrid) utatumika katika mikutano ijayo kwa kuruhusu ushiriki wa wanahisa moja kwa moja au kwa njia ya mtandao.

5.19 ILIRIPOTIWA kuwa Wanahisa walitoa MAAGIZO yafuatayo kufuatia maoni yaliyotolewa hapo awali:

5.19.1 Kuboresha taarifa zilizopo katika daftari la Wanahisa kwa kuhakikisha kuwa taarifa za majina, mawasiliano na malipo ya gawio kwa wanahisa zinawekwa sawa.

5.19.2 Kuboresha utendaji wa Benki kwa ujumla na kutekeleza miradi iliyopangwa ili kuiwezesha Benki kulipa gawio katika Mkutano Mkuu ujao wa Mwaka.

5.19.3 Kuongeza jitihada za kufikia viwango vya kisheria vilivyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) hususan uwiano wa mikopo chechefu (NPL) na uwiano wa gharama kwa mapato (CIR), ili kuwezesha ulipaji wa gawio katika Mkutano Mkuu ujao.

5.19.4 Kuchunguza na kuwekeza katika fursa za kibiashara zilizopo sokoni katika maeneo kama Ifakara na Njombe, pamoja na kuchunguza maeneo mengine ya biashara katika utoaji wa huduma na bidhaa kwa wanafunzi, vijana na sekta isiyo rasmi.

5.19.5 Kuelimisha na kuhamasisha Kanisa na taasisi zake kuanza kutumia Benki na njia zake za utoaji huduma katika kufanikisha miamala mbalimbali.

5.19.6 Kuhakikisha kuwa vifaa vya Mkutano Mkuu wa Mwaka vinatayarishwa kwa wingi na kutolewa kwa Wanahisa wote mapema ili kurahisisha ushiriki mzuri wakati wa mkutano.

5.19.7 Kushughulikia changamoto zilizobainishwa katika jukwaa la benki mtandao (Internet Banking), huduma za uwakala pamoja na kuboresha ufanisi wa utoaji huduma katika matawi yote ya Benki.

5.19.8 Kuzingatia uwezekano wa kuendesha Mkutano Mkuu ujao kwa mfumo wa mseto (yaani mtandaoni na ana kwa ana) ili kuruhusu ushiriki mpana zaidi wa Wanahisa.

5.19.9 Kuzingatia mzunguko wa eneo la kufanyika kwa mkutano mkuu wa mwaka katika mikoa muhimu kama Mwanza, Dodoma na Arusha ili kurahisisha ushiriki wa wanahisa kutoka mikoani.

5.20 Wanahisa wa Benki walipokea, kujadili na kuidhinisha taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.

## 6.0 KUPOKEA, KUJADILI NA KUIDHINISHA TAARIFA YA HESABU ZA BENKI PAMOJA NA TAARIFA YA MKAGUZI WA NJE KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2023.

6.1 ILIRIPOTIWA kuwa mkaguzi wa nje wa Benki kwa mwaka 2023 alikuwa kampuni ya PricewaterhouseCoopers (PwC).

6.2 ILIELEZWA kuwa kufikia tarehe 31 Desemba 2023, wakaguzi waliweza kupitia taarifa ya mizania ya Benki, mapato, taarifa za mabadiliko kwenye hisa zisizo na riba, taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka, muhtasari wa sera pamoja na maelekezo mengine ya kifedha kutoka mwaka uliopita.

6.3 ILIRIPOTIWA kuwa kwa maoni ya wakaguzi, taarifa za fedha zilizokaguliwa zilionesha kwa usahihi hali ya kifedha ya Benki kufikia tarehe 31 Desemba 2023, kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha (IFRS) pamoja na matakwa ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

6.4 ILIELEZWA kuwa ukaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu (ISAs).

6.5 ILIRIPOTIWA kuwa wakaguzi walipata taarifa na maelezo yote waliyoona kuwa ni muhimu kwa madhumuni ya ukaguzi huo.

6.6 ILIELEZWA kuwa kwa mujibu wa maoni ya wakaguzi, Benki iliweka kumbukumbu sahihi za hesabu, Taarifa ya Wakurugenzi ilikuwa sambamba na taarifa za fedha,

taarifa zinazotakiwa kisheria kuhusu malipo ya wakurugenzi na miamala yao na Benki zilifichuliwa ipasavyo, na taarifa ya hali ya fedha pamoja na taarifa ya faida/rasharasha zililingana na vitabu vya hesabu.

6.7 ILIRIPOTIWA kuwa kwa mujibu wa maoni ya wakaguzi, viwango vya mtaji vilivyowasilishwa na Benki vilikokotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Kanuni za Mtaji wa Mabenki za mwaka 2014 pamoja na maelekezo ya Benki Kuu ya Tanzania.

6.8 Wanahisa WALIAZIMIA kuidhinisha taarifa ya fedha ya Benki pamoja na taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2023.

## 7.0 UTEUZI WA MKAGUZI WA NJE

7.1 ILIRIPOTIWA kuwa katika Mkutano Mkuu wa 13 wa Mwaka uliofanyika tarehe 30 Julai 2021, Wanahisa waliamua kuteua kampuni ya PricewaterhouseCoopers (PwC) Tanzania kama wakaguzi wa nje wa Benki kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2022 hadi 2024.

7.2 ILIELEZWA kuwa PwC Tanzania walifanya ukaguzi wa taarifa za fedha za Benki kwa mwaka 2023 na wataendelea kuwa wakaguzi wa nje wa Benki kwa kipindi kilichosalia.

7.3 Wanahisa waliombwa kutambua kuendelea kwa PwC Tanzania kama wakaguzi wa nje wa Benki, ambao pia watafanya ukaguzi wa Benki kwa mwaka 2024.

7.4 Wanahisa WALIAZIMIA kuidhinisha kuendelea kwa kampuni ya PwC Tanzania kama wakaguzi wa nje wa Benki kwa mwaka 2024.

## 8.0 KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA MWAKA UNAOFUATA

8.1 ILIRIPOTIWA kuwa Wanahisa WALIAZIMIA kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao utafanyika tarehe 26 Julai 2025.

## 9.0 MENGINEYO

9.1 ILIRIPOTIWA kuwa Mwenyekiti wa Bodi aliwashukuru Wanahisa kwa ushiriki wao na kuhudhuria mkutano.

9.2 ILIRIPOTIWA kuwa Mwenyekiti aliomba Katibu wa Mkutano asome maazimio ya mkutano kwa ajili ya maoni na uidhinishaji wa Wanahisa.

9.3 ILIRIPOTIWA kuwa Katibu wa Mkutano alisoma maazimio yote yaliyopitishwa wakati wa mkutano, na yote YALIIDHINISHWA na Wanahisa kama yalivyowasilishwa.

## 10.0 KUFUNGA MKUTANO

10.1 Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 8:08 mchana.

**IMETHIBITISHWA TAREHE 26 JULAI 2025**

Mr. Gasper Njuu
**MWENYEKITI**

Ms. Paulina Kunjumu
**KATIBU**

# YATOKANAYO NA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KUMI NA TANO

## AJENDA NAMBA 4

## YALIYOJITOKEZA KATIKA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA 15 ULIOFANYIKA TAREHE 27 JULAI, 2024

| KUMB. NA. | MAELEKEZO YA WANAHISA AU MAOMBI YANAYOTAKIWA KUBORESHWA | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|
| 5.19.1 | Kuboresha rekodi za taarifa katika rejista ya wanahisa kwa kuhakikisha kuwa maelezo ya majina ya wanahisa, mawasiliano yao, na malipo ya gawio ni ya sasa na yameboreshwa. | Benki imeboresha utendaji katika kitengo maalumu kinachohusiana na maswala ya Wanahisa, kwa kuhakikisha kwamba taarifa muhimu za wanahisa zinaboreshwa. Benki inatumia nafasi katika Mkutano Mkuu wa Wanahisa kuboresha taarifa za wahanisa hasa kwa wale wanaoshiriki katika mkutano huo. Baada ya Tangazo la Gawio lilitolewa tarehe 19 Mei 2025, benki imekua ikihimiza wahanisa kuboresha taarifa zao kwa kupitia matawi yetu na njia nyingine mbadala ili kuwezesha malipo ya gawio. Mikakati hii itaboresha kwa kiasi kikubwa taarifa za wanahisa katika rejista. |
| 5.19.2 | Kuboresha utendaji wa benki kwa ujumla na utekelezaji wa miradi iliyopangwa ili benki iweze kuwa katika nafasi ya kulipa gawio katika Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao. | Benki imeboresha kwa kiasi kikubwa utendaji wake katika vigezo vyote muhimu kwa mwaka wa fedha 2024. Tunafuraha kuthibitisha kuwa, kutokana na mafanikio haya, benki iko katika nafasi ya kulipa gawio na tayari imetangaza gawio hilo ambalo litalipwa mwezi Agosti 2025 baada ya Mkutano Mkuu wa Mwaka. |
| 5.19.3 | Kuhimiza juhudi zaidi za kutekeleza viwango vya kisheria vinavyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (NPL na CIR) ili kuiwezesha benki kulipa gawio katika Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao. | Tunayo furaha kuripoti maendeleo makubwa ambapo benki imeboresha uwiano wa gharama kwa mapato (CIR) kutoka asilimia 62 hadi asilimia 57, juu kidogo ya kiwango cha udhibiti cha asilimia 55, na uwiano wa mikopo chechefu (NPL) kutoka asilimia 8 hadi asilimia 3.8, kiwango ambacho kiko ndani ya kigezo cha sekta cha asilimia 5. Ni kutokana na matokeo haya chanya ambapo Benki Kuu ya Tanzania iliidhinisha malipo ya gawio kwa mwaka wa fedha 2024. |

| KUMB. NA. | MAELEKEZO YA WANAHISA AU MAOMBI YANAYOTAKIWA KUBORESHWA | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|
| 5.19.4 | Benki kutafiti fursa za biashara zilizopo sokoni katika maeneo kama Ifakara, Njombe, pamoja na miradi mingine ya biashara inayolenga utoaji wa huduma na bidhaa kwa wanafunzi, vijana, na sekta isiyo rasmi ya biashara. | Benki imeimarisha mkakati wake wa usajili na usimamizi wa wateja wa kibiashara, kwa kulenga soko lake mahususi (yaani Kanisa na Taasisi zake). Kwa sasa, tunatekeleza kwa kasi suluhisho za kimkakati kwa makundi mbalimbali ya wateja muhimu kama Parokia na minyororo yao ya thamani, Hospitali, Taasisi za Elimu ya Juu, na Shule. Tumeimarisha bidhaa ya akaunti ya mwanafunzi kwa kuiongezea vipengele vinavyovutia na vyenye urahisi wa matumizi, ikiwa ni sehemu ya mkakati mpana wa kukuza tabia ya matumizi ya huduma za kibenki kwa vijana, na hasa kujenga kwa muda mrefu thamani ya chapa ya Mkombozi Bank kwa kizazi hiki. Vilevile, tumepanua wigo wa bidhaa zetu za mikopo kwa kuanzisha bidhaa mpya ya “Mikopo Midogo” inayolenga wafanyabiashara binafsi wanaohama kutoka kwenye kundi la Mikopo ya Vikundi vya Umoja, yaani, Solidarity Group Loans (SGL). |
| 5.19.5 | Kuelimisha Kanisa na taasisi zake kutumia benki pamoja na njia zake mbalimbali katika kushughulikia miamala mbalimbali. | Hii ni juhudi ya kimkakati inayoendelea na ambayo inazidi kupata mafanikio kila siku. Tumeanzisha bidhaa na suluhisho muhimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya makundi mbalimbali ya wateja walioko chini ya mwavuli wa Kanisa. Sambamba na hilo, tumeimarisha uwezo wetu wa usambazaji wa huduma zetu kidijitali kama vile Wakala wa Mkombozi, Huduma za Kibenki kwa Njia ya Mtandao, na Huduma za Kibenki kwa Simu. Ndoto zetu za ukuaji wa kimkakati na faida zimejengwa juu ya mwavuli wa Kanisa kama soko maalum, hivyo utekelezaji wa mikakati yetu utaendelea kujikita katika msingi huu muhimu |
| 5.19.6 | Benki kuhakikisha kwamba nyaraka za Mkutano Mkuu wa Mwaka zinaandaliwa kwa idadi ya kutosha na kutolewa kwa wanahisa wote kwa wakati unaofaa ili kurahisisha ushiriki mzuri wakati wa mkutano. | Bodi ya Wakurugenzi inatambua maelekezo yaliyotolewa na Wanahisa kuhusu idadi ya nyaraka za Mkutano Mkuu wa Mwaka, na imehakikisha kuwa nyaraka za Mkutano wa 16 zimeandaliwa kwa ajili ya kuwahudumia Wanahisa wote watakaohudhuria mkutano, huku nyaraka hizo zikipatikana wiki tatu kabla ya mkutano. |

| KUMB. NA. | MAELEKEZO YA WANAHISA AU MAOMBI YANAYOTAKIWA KUBORESHWA | HATUA ZILIZOCHUKULIWA |
|---|---|---|
| 5.19.7 | Benki izingatie mzunguko wa maeneo ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kwa mikoa mikuu kama Mwanza, Dodoma, na Arusha ili kurahisisha ushiriki wa wanahisa kutoka maeneo ya mikoa. | Bodi ya Wakurugenzi imetambua maoni yaliyotolewa na Wanahisa na itazingatia kuandaa mkutano katika mikoa mingine ya nchi baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa gharama zinazohusiana na kuandaa mkutano nje ya Dar es Salaam pamoja kuzingatia ushiriki wa Wanahisa. Uchambuzi huo utatoa mwanga kuhusu mahali pa kuandaa Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao. |
| 5.19.8 | Benki izingatie kuandaa Mkutano Mkuu wa Mwaka ujao kwa mtindo mchanganyiko wa mtandaoni na wa ana kwa ana ili kuwezesha ushiriki mpana wa Wanahisa katika mkutano | Bodi ilitambua maoni ya Wanahisa na itazingatia kuandaa mikutano mchanganyiko katika kupanga Mikutano ya Mwaka ya baadaye ili kuwezesha ushiriki wa wanachama kwa njia ya ana kwa ana na mtandaoni. |
| 5.19.9 | Benki itashughulikia changamoto zilizobainika kwenye huduma za Benki Mtandaoni, huduma za Benki kwa Wakala, pamoja na kuboresha ufanisi wa utoaji wa huduma katika matawi yote ya benki. | Benki imefanya maboresho makubwa katika njia zake za kidijitali, ikiwa ni pamoja na Benki Mtandaoni, Benki kwa Wakala, na Benki kwa Simu. Maboresho haya yameunganishwa na sahihisho la hivi karibuni la Mfumo Mkuu wa Benki, ambalo limechangia kuimarisha utulivu na utendaji wa mfumo. Matokeo yake, umeonekana uboreshaji mkubwa katika ufanisi wa utoaji huduma katika matawi yote ya benki na kwenye majukwaa ya kidijitali |

## AJENDA NAMBA 5

## 5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA YA WAKURUGENZI YA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 31, 2024.

### 5.1 KAZI KUU

Kazi kuu ya benki hii ni utoaji wa huduma za kibenki na huduma zinazohusiana na hizo kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania. Hakukuwa na mabadiliko kwenye shughuli za benki katika mwaka huu wa fedha.

### 5.2 MUUNDO WA HISA

Muundo wa mtaji wa hisa unaojadiliwa ni kama ifuatavyo:

**Mtaji ulioidhinishwa**

TZS 50,000,000,000 inayojumuisha hisa 50,000,000 hisa za kawaida zenye thamani ya TZS 1,000 kila hisa mmoja

**Hisa zilizolipiwa**

TZS 22,820,069,500 inayojumuisha hisa za kawaida 23,555,002 kila hisa ikiwa na thamani ya TZS 1,000/=. Sehemu ya hisa hizi zilizotolewa kwa punguzo kama ilivyoonyeshwa katika taarifa ya maelezo nambari 35 ya taarifa za kifedha.

### 5.3 UMILIKI WA HISA

Hadi kufikia Decemba 31, 2024, umiliki wa hisa ulikuwa kama ifuatavyo :

| WAMILIKI | IDADI YA HISA | THAMANI | % YA UMILIKI |
|---|---|---|---|
| Dayosisi za Kanisa la Katoliki na taasisi zake | 7,049,049 | 6,731,213,750 | 29.50% |
| Taasisi nyingine | 2,235,141 | 2,207,832,500 | 9.67% |
| Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC) | 4,133,995 | 4,133,995,000 | 18.12% |
| Watu binafsi | 10,136,817 | 9,747,028,250 | 42.71% |
| **Jumla** | 23,555,002 | 22,820,069,500 | 100.0% |

Hadi Desemba 31, 2023 umiliki wa hisa ulikuwa kama ifuatavyo:

| AINA | IDADI YA HISA | THAMANI | % YA UMILIKI |
|---|---|---|---|
| Dayosisi za Kanisa Katoliki na taasisi zake | 7,049,049 | 6,731,213,750 | 29.50% |
| Taasisi nyingine | 2,235,141 | 2,207,832,500 | 9.67% |
| Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC) | 4,133,995 | 4,133,995,000 | 18.12% |
| Watu binafsi | 10,136,817 | 9,747,028,250 | 42.71% |
| **Jumla** | 23,555,002 | 22,820,069,500 | 100.0% |

## 5.4 WAKURUGENZI

Wakurugenzi wa Bodi waliokuwa madarakani hadi taarifa inatolewa ni:

| JINA | WADHIFA | UMRI | TAALUMA/SIFA | UTAIFA | TAREHE YA UTEUZI/ KUJIUZULU |
|---|---|---|---|---|---|
| Bw. Gasper Njuu | Mwenyekiti | 65 | Diploma ya Juu ya Benki, Stashahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Fedha, Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (MBA) Kimataifa | Mtanzania | Januari 27, 2022 |
| Respige O. Kimati | Mkurugenzi Mtendaji | 51 | Shahada ya Biashara katika Fedha, Shahada ya Uzamili (MSc) katika Fedha | Mtanzania | Januari 18, 2020 |
| Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | Mkurugenzi | 68 | Askofu Mkuu Dayosisi ya Dodoma, Shahada ya Uzamili katika Historia, Shahada ya Jiografia, Shahada ya Theolojia | Mtanzania | Aliteuliwa tena Mei 30, 2015 |
| Bw. Martin Mdoe | Mkurugenzi | 54 | Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Shahada ya Sheria (LLB), Shahada ya Juu ya Sheria (LLM) na Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (MBA). | Mtanzania | Januari 27, 2022 |
| Bw. Robert Mtendamema | Mkurugenzi | 52 | Shahada ya Sayansi ya Kompyuta na Shahada ya Uzamili ya Sayansi Mifumo ya Mawasiliano ya Data. | Mtanzania | Agosti 8, 2018 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Bi. Uphoo Swai | Mkurugenzi | 53 | Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa (CPA), Diploma ya Juu ya Uhasibu, Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara. | Mtanzania | Agost 8, 2018 |
| Bw. Benedict Warisianga Sudi | Mkurugenzi | 57 | Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa (CPA), Diploma ya Juu ya Uhasibu. | Mtanzania | Mei 9, 2019 |
| Padri. Dk. Charles Kitima | Mkurugenzi | 60 | Shahada ya Sanaa katika Theolojia, Leseni katika Sheria za Canon na Shahada ya Uzamivu ya Sheria. | Mtanzania | Januari 2, 2019 |

**Wakurugenzi wafuatao wanamiliki hisa hadi kufikia mwaka huu:**

| Jina la mkurugenzi | Idadi ya hisa | |
|---|---|---|
| | 2024 | 2023 |
| Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | 13,574 | 13,574 |
| Bw. Robert Mtendamema | 1,190 | 1,190 |
| Bw. Respige Kimati | 260 | 260 |
| **Jumla ya hisa zinazomilikiwa na wakurugenzi** | **15,024** | **15,024** |

Hakuna mkurugenzi aliyemiliki zaidi ya asilimia 0.1 ya hisa za mtaji zilizotolewa na Benki.

## 5.5 KATIBU WA KAMPUNI

Hadi kufikia Desemba 2024, Katibu wa Benki alikuwa ni Bi. Paulina Kunjumu.

## 5.6 UONGOZI WA KAMPUNI

Bodi ya Wakurugenzi (”Bodi”) ina wajumbe wanane, wakiwemo Mkurugenzi Mtendaji. Mbali na Mkurugenzi Mtendaji, hakuna Mkurugenzi anayeshikilia wadhifa wa kiutendaji ndani ya benki. Bodi ina jukumu la kusimamia Benki kwa jumla, kama vile kutambua maeneo ya hatari muhimu, kufuatilia maamuzi ya uwekezaji, kuangalia masuala makubwa ya kifedha, na kupitia utendaji wa uongozi dhidi ya mipango ya biashara na bajeti.

Bodi pia inahakikisha kuwepo kwa mfumo mzuri wa sera na taratibu za udhibiti wa ndani zinazofuata kanuni za utawala bora wa kampuni.

Bodi inapaswa kukutana angalau mara nne kwa mwaka. Wajumbe wa Bodi watakasimu shughuli za kila siku za uongozi kwa Mkurugenzi Mtendaji ambaye atasaidiama ma timu yake ya uongozi. Timu hii hualikwa kuhudhuria mikutano ya Bodi na kusaidia kudhibiti shughuli za Benki kwa ufanisi, na pia kuwasiliana na kuratibu kati ya vitengo mbalimbali vya biashara.

Katika mwaka huu, Bodi ilifanya mikutano minne ya kawaida na mitano ya dharura kwa sababu za shughuli maalum zinazohitaji majadiliano ya Bodi. Hapa chini ni muhtasari wa mikutano iliyofanyika mwaka huu;

| Na. | Jina la Mkrugenzi | Cheo | Idadi ya Mikutano | Mikutano aliyohudhuria | Mahudhurio |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Gasper Njuu | Mwenyekiti wa Bodi | 9 | 9 | 100% |
| 2. | Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | Mkurugenzi | 9 | 9 | 100 % |
| 3. | Bw. Benedict Sudi | Mkurugenzi | 9 | 9 | 100% |
| 4. | Bw. Robert Mtendamema | Mkurugenzi | 9 | 9 | 100% |
| 5. | Bi. Uphoo Swai | Mkurugenzi | 9 | 8 | 89% |
| 6. | Padre Dk. Charles Kitima | Mkrugenzi | 9 | 8 | 89% |
| 7. | Bw. Martin Mdoe | Mkurugenzi | 9 | 9 | 100% |

Bodi ina kamati tatu, ambazo ni Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi; Kamati ya Rasilimali Watu na Uendeshaji na Kamati ya Mikopo. Kila kamati ina mkataba wa kazi unaoelezea majukumu yake na kusaidia kuhakikisha ufanisi wa utendaji wa Bodi.

Benki inajitahidi kufuata kanuni za utawala bora wa kampuni, hasa kutambua umuhimu wa uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Bodi inasimamia kwa karibu shughuli za Benki na kuhakikisha viwango vya juu vya utawala bora kupitia kamati zake kama ifuatavyo:

### Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi inaundwa na wajumbe wafuatao:

| No. | Jina la mkurugenzi | Cheo | Idadi ya mikutano | Mikutano alyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Uphoo Swai | Mwenyekiti | 6 | 6 | 100% |
| 2. | Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya | Mjumbe | 6 | 6 | 100% |
| 3. | Bw. Benedict Sudi | Mjumbe | 6 | 6 | 100% |

### Kamati ya Bodi ya Mikopo inaundwa na wajumbe wafuatao:

| No. | Jina la mkurugenzi | Cheo | Idadi ya mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Robert Mtendamema | Mwenyekiti | 24 | 24 | 100% |
| 2. | Bw. Martin Mdoe | Mjumbe | 24 | 24 | 100% |
| 3. | Padri. Charles Kitima | Mjumbe | 24 | 24 | 100% |

### Kamati ya Rasilimali watu na Uendeshaji inaundwa na wajumbe wafuatao:

| No. | Jina la mkurugenzi | Cheo | Idadi ya mikutano | Mikutano aliyohudhuria | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Martin Mdoe | Mwenyekiti | 9 | 9 | 100% |
| 2. | Bw. Robert Mtendamema | Mjumbe | 9 | 8 | 89% |
| 3. | Padri Charles Kitima | Mjumbe | 9 | 9 | 100% |

## 5.7 MENEJIMENTI

Mkurugenzi Mtendaji alisaidiwa na wakuu wa idara kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| • Afisa Mkuu wa Fedha<br>• Afisa Mwendeshaji Mkuu<br>• Mkuu wa Hazina<br>• Mkuu wa Mikopo<br>• Mkaguzi wa Ndani<br>• Afisa Biashara Mkuu | • Mkuu wa idara ya sheria (Katibu wa Kampuni)<br>• Mkuu wa Idara ya Ukubalifu na Vihatarishi<br>• Mkuu wa Rasilimali Watu<br>• Mkuu wa Kitengo cha Tehama na Mifumo |

Taarifa zaidi za utendaji zimo kwenye aya ya 5.8 kwenye taarifa ya wakurugenzi.

## 5.8 UTENDAJI WA KIFEDHA NA HALI YA BENKI

Benki ilipata faida kabla ya kodi ya TZS 11,493 milioni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 (2023: TZS 8,572 milioni), ambayo ilitokana na vigezo muhimu vya utendaji kama ifuatavyo: -

- Mapato halisi ya uendeshaji kwa kipindi hicho yalikuwa TZS 29,216 milioni, ikilinganishwa na TZS 25,226 milioni mwaka 2023. Ukuaji huu ulisababishwa hasa na ongezeko la mapato ya riba kwa TZS 4,631 milioni (26%). Hii ilitokana na mizania iliyo imara na salama na kupungua kwa 5% (TZS 361 milioni) kwa gharama za riba kupitia usimamizi mzuri wa mchanganyiko wa amana.

- Amana za wateja ziliongezeka hadi TZS 217,491 milioni (2023: TZS 207,397 milioni), zikionyesha ukuaji wa 5% mwaka 2024, kutokana na jitihada za ukusanyaji wa amana na kuboresha miundombinu ya benki ikiwemo njia za kidijitali.
- Jumla ya Mali za Benki ziliongezeka hadi TZS 282,380 milioni (2023: TZS 255,789 milioni). Kwa kiasi kikubwa ongezeko hili lilitokana na ongezeko la TZS 28,304 milioni katika mikopo ya wateja na taasisi za fedha. Ongezeko hili likilinganishwa na kipindi kilichotangulia linaonyesha uwezo ulioboreshwa wa benki kutoa mikopo na ukuaji wa wateja.
- Gharama za uendeshaji jumla ziliongezeka hadi TZS 17,723 milioni, ikilinganishwa na TZS 16,654 milioni mwaka 2023. Kuongezeka kwa 6% kunatokana na upanuzi wa biashara na kiwango kikubwa cha shughuli za uendeshaji.
- Mikopo kwa wateja iliongezeka hadi TZS 162,565 milioni (2023: TZS 134,261 milioni), ikionyesha ongezeko la 21% mwaka 2024. Ukuaji huu unatokana hasa na mchakato ulioboreshwa wa utoaji mikopo na hali bora ya utoshelevu wa mtaji ikilinganishwa na kipindi kilichotangulia.

Vigezo muhimu vya utendaji (KPIs) vya Benki vimeonyeshwa hapa chini:

| Kiashiria cha Utendaji | Tafsiri na njia ya kufanya hesabu | 2024 | 2023 |
|---|---|---|---|
| Mapato kwa Kila Hisa | Faida/(Hasara) Kabla ya Kodi/Jumla ya Hisa | 29% | 28% |
| Uwiano wa Mapato na Mali | Faida/(Hasara) Kabla ya Kodi/Jumla ya Mali | 4% | 3% |
| Uwiano wa Gharama na Mapato | Gharama za Uendeshaji/Mapato halisi ya Riba na Yasiyo ya Riba | 57% | 62% |
| Uwiano wa Riba inayotozwa na Benki na ile inayolipwa kwa mteja ikilinganishwa na Mali zinazozalisha fedha | Mapato yote ya Riba/ (Riba inayopatikana kutokana na amana za serikali + Salio katika benki nyingine + Mikopo iliyopokelewa kutoka benki nyingine + Uwekezaji katika Amani nyinginezo + Mikopo) | 13% | 12% |
| Uwiano wa Mapato yasiyo ya riba na Mapato Ghafi | Mapato Yasiyo ya Riba/Mapato Yote | 28% | 26% |
| Uwiano Mapato kwa kila Hisa | Mapato ya Msingi/Idadi ya Hisa za kawaida kwa Shilingi za Tanzania | 384% | 324% |
| Uwiano wa Mikopo yote na Amana za wateja | Jumla ya Mikopo kwa Wateja/ Jumla ya Amana za Wateja | 75% | 67% |
| Uwiano wa Mikopo Chechefu na Mikopo Yote | Mikopo Chechefu/Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.8% | 8% |
| Mali inayoingiza Mapato na Jumla ya Mali | Mali iingizayo Mapato/Mali zote | 81% | 82% |
| Ukuaji wa Mali | Mwenendo (Jumla ya Mali 2024 – Jumla ya Mali 2023) | 10% | 16% |

| Utoshelevu wa Mtaji | | | |
|---|---|---|---|
| Uwiano wa Mtaji Msingi (Kundi la Kwanza) | [Mtaji Mkuu/ Jumla ya Kiwango vihatarishi tarajiwa katika Hali ya Kifedha ya Benki, Kiwango cha ukosefu wa kinga kwa Benki juu ya Vihatarishi vya kiutendaji na vya sokoni x 100 | 16.93% | 13.7% |
| Uwiano wa Mtaji wa Jumla + Kundi la Pili) | [Jumla ya Mtaji/Jumla Kiwango cha Vihatarishi/ mali zilizo wazi kwenye taarifa ya fedha na zile ambazo hazijawekwa wazi, kiasi cha hatari zinazotokana na shughuli za ndani] x 100 | 18.23% | 15.28% |

Kiwango cha Mtaji Msingi na Kiwango Jumla cha Mtaji kilikuwa TZS milioni 35,319 na TZS milioni 38,019, sawa na asilimia 16.93 na 18.23 mtawalia (2023: TZS milioni 23,880, asilimia 13.73 na 15.28). Mwaka huu, viwango hivi vimezidi mahitaji ya chini ya kisheria ya TZS milioni 15,000, pamoja na asilimia 12.5 na 14.5 mtawalia huo kwa Kiwango cha Mtaji Msingi na Kiwango Jumla cha Mtaji. Wakurugenzi wanathibitisha kuwa viwango vinavyotumika vya uhasibu vimezingatiwa na taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuzingatia kuendelea kwa shughuli za kampuni.

## 5.9 MITANDAO NA MATAWI YA BENKI

Benki ilikuwa na jumla ya matawi kumi na tatu hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2024; manne yakiwa Dar es Salaam, mawili Mwanza, na tawi moja katika kila mji wa Bukoba, Morogoro, Dodoma, Iringa, Njombe, Moshi na Arusha. Idadi ya jumla ya wateja wa amana na wakopaji wa benki hiyo hadi mwisho wa mwaka husika ilikuwa kama inavyoonyeshwa hapa chini:

| | 2024 | 2023 |
|---|---|---|
| **Aina ya Akaunti** | | |
| Akaunti za Hundi | 6,335 | 5,406 |
| Akaunti za Akiba | 166,276 | 112,144 |
| Akiba za Muda Maalum | 844 | 981 |
| **Jumla ya Akaunti** | **173,455** | **118,531** |
| **Idadi ya wateja wakopaji** | **12,143** | **16,155** |

## 5.10 GAWIO

Wakurugenzi wanapendekeza ulipaji wa gawio kwa mwaka wa kwa kiwango cha TZS 92.40 kwa kila hisa (2023: Hakukuwa na gawio)

## 5.11 MAMBO MUHIMU YALITOKEA MWAKA 2024

- Tumefanikiwa kutekeleza mfumo mpya wa Msingi wa Kibenki (RUBIKON) na kukamilisha uhamishaji wa shughuli zote za huduma za kibenki pamoja na njia zote za utoaji huduma kwenda kwenye mfumo mpya.
- Mradi wa Mfumo wa Usimamizi wa Shule umekamilika na utekelezaji wake umeanza, kwa lengo la kufikia shule 200 ifikapo mwisho wa mwaka 2026.
- Utekelezaji wa suluhisho za kidijitali unaendelea kupata mwitikio mzuri. Njia yetu ya Wakala wa Benki (Mkombozi WAKALA), Suluhisho la Usimamizi wa Mapato ya Kanisa (SADAKA Digital), Huduma ya Benki kwa Njia ya Mtandao na Benki ya Simu vimeendelea kupata ukuaji mkubwa katika matumizi na usambazaji kwa wateja.
- Tumetekeleza mradi wa kuoanisha matumizi ya ATM kati ya Benki ya NMB na Umoja Switch, hatua ambayo inawawezesha wateja wa benki yetu kupata huduma za kutoa fedha kupitia mtandao wa ATM za Benki ya NMB.
- Tumeanzisha Suluhisho la Usimamizi wa Fedha katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) kwa ajili ya ukusanyaji wa ada, na tunapanga kupeleka huduma hii katika taasisi nyingine za elimu ya juu ndani ya soko letu mahususi.
- Mfumo wa Usimamizi wa Hospitali umekamilika na kwa sasa uko kwenye hatua ya kuunganishwa katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando. Tunatarajia kuusambaza pia kwa vituo vingine vya afya ndani ya soko letu mahususi.
- Tumeanza maandalizi muhimu kwa ajili ya kupanua mtandao wa matawi ya benki, kwa lengo la kufungua matawi mapya katika mwaka 2025 kulingana na mpango mkakati wa benki.

## 5.12 MIAMALA NA WANAOHUSIANA NA BENKI

Miamala na salio kwa wahusika vimewekwa katika kiambatisho 38 cha taarifa za fedha.

## 5.13 MIPANGO YA MAENDELEO

Benki inaendelea kuelekeza nguvu zake katika utekelezaji wa mikakati yake ya msingi kwa kipindi kifupi na cha kati, kwa lengo la kufikia viwango endelevu vya faida vinavyohitajika kwa ajili ya ukuaji na kutoa gawio kwa wanahisa. Tutaendelea kujielekeza katika kupenya zaidi kwenye soko kwa kutoa huduma za kibenki zenye ushindani, sambamba na kutumia kikamilifu fursa zilizopo kwa wateja wetu wa sasa, hususan walioko katika soko letu mahususi.

## 5.14 RASILIMALI WATU

Benki ina idadi ya kutosha ya wafanyakazi wenye ujuzi na uzoefu unaohitajika katika nafasi muhimu za kazi kwa ajili ya kusimamia shughuli za kibenki na kufanikisha malengo ya biashara.

## 5.15 VIHATARISHI VIKUU NA MAMBO YANAYOLETA WASIWASI

### Mfumo wa Usimamizi wa Hatari

Hatari kuu zinazokabili Benki hutokana na kutoa mikopo kwa wateja kupitia shughuli zetu za biashara na ukopeshaji. Benki pia inakabiliwa na aina nyingine za vihatarishi kama vya soko, ukwasi, uendeshaji, sifa na hatari zingine zinazojitokeza kutokana na mkakati wa Benki, aina za bidhaa na usambazaji wa kijeografia. Usimamizi mzuri wa vihatarishi ni msingi wa kupata faida kwa njia endelevu na hivyo ni sehemu muhimu ya usimamizi wa kifedha na uendeshaji wa Benki.

### Usimamizi wa Vihatarishi

Jukumu kuu la kuweka kiwango cha hatari kinachokubalika na kusimamia hatari ni la Bodi ya Wakurugenzi. Kwa mamlaka waliyopewa na Bodi, Kamati ya Ukaguzi, na usimamizi wa Vihatarishi inasimamia na kupitia hatari mbalimbali ikiwemo mikopo, soko, mtaji, uhaba wa fedha na matatizo ya uendeshaji. Kamati hupitia kiwango cha jumla cha hatari na kutoa mapendekezo kwa Bodi.

Kamati pia hupitia mifumo ya usimamizi wa hatari na udhibiti wa Benki, kuchambua mabadiliko makubwa ya kanuni, na kuhakikisha ukaguzi mzuri wa miamala mikubwa. Kamati hupokea ripoti za mara kwa mara kuhusu usimamizi wa hatari, sera, majaribio ya msukosuko, uhaba wa fedha, na ufanisi wa mtaji, na inaweza kuchunguza au kupata taarifa kuhusu shughuli yoyote ndani ya majukumu yake.

Bodi ina jukumu la mwisho la kusimamia vihatarishi na mifumo ya udhibiti wa ndani ya Benki. Wakurugenzi wanahakikisha mifumo ya udhibiti wa kifedha na uendeshaji inatengenezwa na kudumishwa kila wakati. Ufanisi wa mifumo hii unategemea utekelezaji wa kanuni zilizowekwa. Hata hivyo, kuna hatari ya kutotii kanuni hizo kwa wafanyakazi. Ingawa hakuna mfumo unaoweza kutoa uhakika kamili dhidi ya makosa au hasara, mfumo wa Benki umeundwa kutoa uhakika wa kutosha kwa Bodi kwamba taratibu zinafanya kazi vizuri.

Bodi ilikagua mifumo ya udhibiti wa ndani mwaka wa fedha ulioishia 31 Desemba 2024 na inaamini imekidhi vigezo vilivyokubaliwa. Ukaguzi wa vihatarishi na mifumo ya udhibiti wa ndani hufanywa kupitia Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi ya Bodi.

### Utamaduni wa Usimamizi wa Vihatarishi

Benki inatambua kuwa watu ni rasilimali yake muhimu na ni muhimu kuanzisha utamaduni mzuri wa usimamizi wa vihatarishi. Kwa hiyo, Benki inaendelea kuwekeza katika uwezo wa wafanyakazi wake kupitia mipango maalum ili kuimarisha utamaduni huu. Majukumu ya usimamizi wa vihatarishi yamefafanuliwa katika safu tatu za ulinzi:

- **Safu ya Kwanza ya Ulinzi:** Hii inajumuisha usimamizi na udhibiti wa dani; mameneja wa operesheni wanamiliki na kusimamia vihatarishi. Pia, wanawajibika kutekeleza hatua za marekebisho kushughulikia kasoro za mchakato na udhibiti.
- **Safu ya Pili ya Ulinzi:** Kitengo huru cha vihatarishi kinahakikisha vihatarishi vinaendelea kuwa ndani ya kiwango kinachokubalika.
- **Safu ya Tatu ya Ulinzi:** Idara huru ya Ukaguzi wa Ndani inayosimamiwa na Kamati ya Ukaguzi ya Bodi.

## 5.16 USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA USIMAMIZI WA MIFUMO YA NDANI

Bodi inachukua jukumu la mwisho la kusimamia vihatarishi na mifumo ya udhibiti wa ndani ya Benki. Wakurugenzi wanahakikisha kwamba mifumo ya udhibiti wa kifedha na shughuli za ndani inatengenezwa na kudumishwa kila wakati ili kutoa uhakikisho wa kutosha kuhusu:

- Ufanisi na uendeshaji mzuri wa shughuli za kibenki;
- Ulinzi wa mali za Benki;
- Kufuata sheria na kanuni zinazotumika;
- Uhakika wa rekodi za uhasibu;
- Uendelevu wa biashara katika hali za kawaida na changamoto; na
- Kuwa na tabia nzuri na kuwajibika kwa wadau wote.

Ufanisi wa mfumo wowote wa udhibiti wa ndani unategemea kufuata kwa makini hatua zilizowekwa. Daima kuna hatari ya wafanyakazi kutofuatilia hatua hizi. Ingawa hakuna mfumo unaoweza kuzuia kabisa makosa au hasara, mfumo wa Benki umeundwa kutoa uhakikisho wa kutosha kwa Bodi kwamba taratibu zinazotumika zinafanya kazi vizuri. Bodi ilipima mifumo ya udhibiti wa ndani mwaka mzima wa fedha na inaamini kuwa ilikidhi vigezo vilivyokubaliwa. Bodi inafuatilia hatari na ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani kupitia Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi pamoja na Kamati ya Mikopo ya Bodi.

## 5.17 MASUALA MAKUBWA YANAYOWEZA KULETA MADHARA

Kwa maoni ya Bodi hakuna masuala ya kisheria ambayo yanaweza kuathiri utendaji wa benki.

## 5.18 USTAWI WA WAFANYAKAZI

### Uhusiano kati ya Menejimenti na wafanyakazi

Uhusiano kati ya wafanyakazi na uongozi umeendelea kuwa mzuri. Malalamiko hutatuliwa kupitia mikutano na mazungumzo. Morali ya kazi bado ni nzuri na hakukuwa na malalamiko yoyote ambayo hayajatatuliwa. Kulikuwa na ushirikiano mzuri kati ya menejimenti na wafanyakazi.

Benki ni mwajiri anayewatendea wafanyakazi wote kwa usawa. Inatoa fursa sawa za ajira na kuhakikisha mtu bora anateuliwa kwa nafasi yoyote bila ubaguzi wa aina yoyote, na bila kuzingatia jinsia, hali ya ndoa, kabila, dini, au ulemavu ambao hauathiri uwezo wa mtu kufanya kazi zake.

### Mafunzo

Katika mwaka huo, Benki ilitumia Shilingi milioni 63.7 kwa mafunzo ya wafanyakazi (2023: Shilingi milioni 87.6). Mpango wa mafunzo umeendelea kuboreshwa ili kuhakikisha wafanyakazi wanapata mafunzo yanayohitajika katika ngazi zote. Wafanyakazi walipata mafunzo ya kuboresha ujuzi wao na kufanya kazi zao vizuri zaidi.

### Mikopo na Misaada kwa Wafanyakazi

Benki hutoa mikopo na malipo kabla ya mwezi kwa wafanyakazi ili kuwasaidia kukidhi mahitaji yao ya kifedha na kukuza maendeleo yao. Mikopo na malipo kabla ya mwezi hutolewa chini ya masharti maalum yaliyopitishwa na Bodi.

### Huduma za Matibabu

Benki inalipia gharama za matibabu kwa wafanyakazi wote na wategemezi wao na kuwapatia bima ya matibabu.

### Mafao ya Kustaafu

Benki hufanya michango ya kisheria kwa ajili ya mafao ya kijamii ya wafanyakazi. Michango ya Benki ni hadi asilimia 10 ya mshahara wa jumla wa mfanyakazi.

## 5.19 USAWA WA KIJINSIA

Benki ni muajiri anayetoa fursa sawa kwa wote kwa kuzingatia usawa wa kijinsia kama ifuatavyo.

| **Jinsia** | **2024** | **2023** |
|---|---|---|
| wanawake | 93 | 82 |
| wanaume | 103 | 103 |
| **Jumla** | **196** | **185** |

## 5.20 MICHANGO YA KISIASA

Benki haikutoa michango yoyote ya kisiasa mwaka (2023: hakuna).

## 5.21 UHUSIANO NA WADAU

Benki inaendelea kuwa na uhusiano mzuri na wadau mbali mbali wakiwemo wasimamizi wa shughuli za kibenki.

## 5.22 WAJIBU WA KIJAMII WA BENKI NA MICHANGO YA HISANI

Benki hushiriki kikamilifu katika shughuli za jamii na mipango ya maendeleo kote nchini. Misaada ya hisani iliyotolewa katika mwaka huo ilikuwa shilingi milioni 19.48 (2023: shilingi milioni 17.25). Benki ilitoa misaada kwa taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na msaada wa elimu kwa watoto yatima.

## 5.23 MKAGUZI WA HESABU ZA BENKI

PricewaterhouseCoopers alikuwa mkaguzi wa hesabu wa Benki kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2024. Pendekezo la kuteua mkaguzi wa hesabu wa nje wa Benki kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2024 lilipitishwa na wanahisa katika Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu wa Mwaka, ambao uliamua kwamba PricewaterhouseCoopers ataendelea kuwa mkaguzi wa hesabu wa Benki kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2022.

Ripoti ya Wakurugenzi ilipitishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 26 Machi, 2025 na kusainiwa kwa niaba ya Bodi kwa mujibu wa azimio la Bodi na:



**BW. GASPER CASMIR NJUU**
**MWENYEKITI WA BODI**

# TAARIFA ZA MAJUKUMU YA WAKURUGENZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA, 2024

Sheria ya Kampuni za mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha za mwaka 2006 ya Tanzania zinawataka wakurugenzi kuandaa taarifa za fedha kwa kila kipindi cha fedha zinazowasilishwa kwa haki, kwa kila jambo muhimu, hali halisi ya mambo ya kifedha ya Benki kufikia mwisho wa mwaka wa kifedha na faida au hasara ya mwaka huo.

Wakurugenzi pia wanawajibika kuhakikisha Benki inaweka rekodi za uhasibu kwa usahihi ambazo zinaonyesha, kwa usahihi unaokubalika, hali ya kifedha ya Benki. Aidha, wanawajibika kulinda mali za Benki.

Wakurugenzi wanakubali kuwajibika kwa taarifa za kifedha za kila mwaka, ambazo zimeandaliwa kwa kutumia sera za uhasibu zinazofaa, zikiungwa mkono na maamuzi na makadirio ya busara na tahadhari, na kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha (IFRS) pamoja na mahitaji ya Sheria ya Kampuni za mwaka 2002 na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania. Wakurugenzi wako na imani kwamba taarifa za kifedha zinaonyesha kwa haki, kwa kila jambo muhimu, hali halisi ya mambo ya kifedha ya Benki na matokeo yake ya kifedha kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha (IFRS) na mahitaji ya Sheria ya Kampuni za mwaka 2002 na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania. Aidha, wakurugenzi wanakubali kuwajibika kwa utunzaji wa rekodi za uhasibu ambazo zinaweza kutegemewa katika maandalizi ya taarifa za kifedha, pamoja na kubuni, kutekeleza na kudumisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaohitajika kwa ajili ya maandalizi na uwasilishaji wa taarifa hizo kwa usahihi bila makosa makubwa.

Wakurugenzi wa Benki wamefanya tathmini ya uwezo wa Benki kuendelea kuwa taasisi hai kwa muda unaotarajiwa na hawana sababu za kuamini kwamba biashara haitakuwa hai mwaka ujao.

Taarifa za kifedha ziliridhiwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 26 Machi, 2025 na zilisainiwa kwa niaba yake na:

**Bw. Gasper Njuu**
**Mwenyekiti wa Bodi**

**Bi. Uphoo Swai**
**Mjumbe wa Bodi na Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vihatarishi**

# TAMKO LA MKUU WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2024

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu (NBAA), kwa nguvu ya Sheria ya Wakaguzi na Wahasibu (Usajili) Na. 33 ya mwaka 1972, iliyorekebishwa na Sheria Na. 2 ya mwaka 1995, inahitaji taarifa za kifedha ziambatanishwe na tamko la Mtendaji wa Fedha anayehusika na maandalizi ya taarifa hizo.

Ni jukumu la Mhasibu Mtaalamu kusaidia Bodi ya Wakurugenzi kuandaa taarifa za kifedha zinazoonyesha kwa uwazi hali ya fedha na matokeo ya taasisi kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha na Sheria ya Kampuni za mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania. Jukumu la kisheria la maandalizi ya taarifa za kifedha lipo kwa Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoelezwa kwenye Tamko la Majukumu ya Wakurugenzi ukurasa uliopita.

Mimi, **Vitalis Constantine Michael**, nikiwa Afisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya Biashara Mkombozi, ninathibitisha kuwa nina jukumu la kuhakikisha taarifa za kifedha za mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2024 zimeandaliwa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha na Sheria ya Kampuni za mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 ya Tanzania.

Ninathibitisha kwamba taarifa za kifedha zinaonyesha kwa uwazi hali ya fedha na matokeo ya Benki ya Biashara Mkombozi kufikia tarehe hiyo na kwa mwaka huo, na kwamba taarifa hizi zimeandaliwa kwa kutumia rekodi za kifedha zilizoandikwa na kuhifadhiwa ipasavyo.

Imesainiwa na:

**Vitalis Constantine Michael**

**Cheo: Ofisa Mkuu wa Fedha**
**Namba ya Uanachama wa NBAA: ACPA 6278**
**Tarehe: Machi, 26, 2025**

## AJENDA YA 6

## KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA TAARIFA ZA KIFEDHA ZA BENKI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DECEMBA, 2024 NA KUPITISHA RIPOTI YA MKAGUZI WA NJE KUHUSU TAARIFA ZA KIFEDHA ZA BENKI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DECEMBA, 2024.

### RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA KIFEDHA

#### Maoni

Tumehakiki taarifa za kifedha za Benki ya Biashara Mkombozi (Benki) zilizopo katika kurasa 50 hadi 78, zikiwemo taarifa ya hali ya kifedha kufikia tarehe 31 Desemba 2024, taarifa ya faida au hasara na mapato mengine, taarifa ya mabadiliko ya mtaji, na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo, pamoja na maelezo ya taarifa za kifedha, ikijumuisha muhtasari wa sera muhimu za uhasibu.

Kwa maoni yetu, taarifa za kifedha zinaonyesha kwa uwazi na haki hali ya kifedha ya Benki ya Biashara Mkombozi kufikia tarehe 31 Desemba 2024, na matokeo yake ya kifedha na mtiririko wa fedha kwa mwaka huo kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IFRS) na Sheria ya Kampuni, Na. 12 ya mwaka 2002.

#### Msingi wa Maoni

Tumeendesha ukaguzi wetu kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISAs). Majukumu yetu chini ya viwango hivyo yameelezwa zaidi katika sehemu ya "Majukumu ya Mkaguzi kwa ukaguzi wa taarifa za kifedha" ya ripoti yetu. Tunaamini ushahidi tulioupata ni wa kutosha na unaofaa kuunga mkono maoni yetu.

Tuko huru na Benki kwa mujibu wa Kanuni za Maadili za Kimataifa kwa Wahasibu Wataalamu (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Uhuru) vilivyotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Maadili kwa Wahasibu (IESBA Code) na mahitaji ya maadili ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu (NBAA) yanayohusiana na ukaguzi wetu Tanzania. Tumejitahidi kutimiza majukumu yetu ya maadili kwa mujibu wa IESBA Code na mahitaji ya NBAA.

### RIPOTI YA MAHITAJI MENGINE YA KISHERIA NA KIDHIBITI

Ripoti hii, ikijumuisha maoni, imetayarishwa kwa ajili ya wanachama wa Benki kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni, Na. 12 ya mwaka 2002, na si kwa madhumuni mengine yoyote.

Kama inavyotakiwa na Sheria ya Kampuni, Na. 12 ya mwaka 2002, tunapaswa kuripoti ikiwa, kwa maoni yetu, ripoti ya wale walio na mamlaka ya kusimamia benki hailingani na taarifa za kifedha, Benki haijahifadhi rekodi za uhasibu ipasavyo, taarifa za kifedha hazilingani

na rekodi za uhasibu, hatukupata taarifa na maelezo yote tuliyohitaji kwa ajili ya ukaguzi wetu, au kama taarifa za kisheria kuhusu malipo kwa wakurugenzi na miamala na Benki hazijafichuliwa. Kuhusu haya, hatuna malalamiko ya kuripoti.

Mshirika wa ukaguzi anayehusika na ripoti hii ya mkaguzi huru ni Cletus Kiyuga.

Cletus Kiyuga ACPA- PP 1981
**Kwa niaba ya PricewaterhouseCoopers**
Certified Public Accountants

Dar es Salaam
26 Machi 2025

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA BENKI HADI DESEMBA 2024

| | Maelezo | 2024<br>TZS'000 | 2023<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|
| Mapato ya riba yaliyohesabiwa kwa kutumia njia ya riba yenye ufanisi | 8 | 30,108,219 | 25,883,140 |
| Gharama ya riba iliyohesabiwa kwa kutumia njia ya riba yenye ufanisi | 9 | (7,702,557) | (8,109,203) |
| **Mapato ya Riba** | | **22,405,662** | **17,773,937** |
| Hasara zinazotarajiwa za mikopo – mali za kifedha | 10 | (1,651,387) | (1,649,509) |
| **Mapato halisi ya riba baada ya hasara zinazotarajiwa za mikopo** | | **20,754,275** | **16,124,428** |
| Mapato ya ada na kamisheni | 11 | 4,252,461 | 4,472,373 |
| Mapato mengine | 12 | 1,405,242 | 1,384,901 |
| Faida halisi baada ya kuondolewa kwa mali za kifedha zilizopimwa kwa thamani ya haki kupitia mapato mengine ya kina | 23(c) | 159,086 | 1,369,354 |
| Faida halisi kutokana na biashara na kubadilisha fedha za kigeni | 13 | 2,645,395 | 1,875,225 |
| **Jumla ya Mapato Yasiyo ya Riba** | | **8,462,184** | **9,101,853** |
| **Faida Halisi ya Uendeshaji** | | **29,216,459** | **25,226,281** |
| Gharama za wafanyakazi | 14 | (9,256,991) | (8,750,332) |
| Uchakavu na upunguzaji wa thamani | 15 | (2,182,975) | (2,162,153) |
| Gharama nyingine za uendeshaji | 16 | (6,283,193) | (5,741,564) |
| **Jumla ya gharama za uendeshaji** | | **(17,723,159)** | **(16,654,049)** |
| **Faida kabla ya Kodi ya Mapato** | | **11,493,300** | **8,572,232** |
| Kodi ya mapato (malipo) | 17 | (2,451,883) | (942,106) |
| **Faida ya Mwaka** | | **9,041,417** | **7,630,126** |
| Mapato mengine | | | |
| ***Vitu vinavyoweza kubadilishwa kisha kuwa faida au hasara*** | | | |
| Hisa za uwekezaji za FVOCI (Thamani ya Haki Kupitia Mapato Mengine ya Kina); | | | |
| -Hasara/faida ya thamani ya haki iliyotokea mwaka huu (Maelezo 23a) | | (273,857) | (2,257,153) |
| -Kodi inayohusiana na hayo<br>Mapato mengine ya kina, baada ya kodi | | 82,157 | 677,146 |
| | | **(191,700)** | **(1,580,007)** |
| **Jumla ya mapato yote ya kina kwa mwaka, baada ya kodi** | | **8,849,717** | **6,050,119** |
| **Faida msingi na faida iliyopunguzwa kwa kila hisa** | **18** | **384** | **324** |

## TAARIFA YA HALI YA FEDHA YA BENKI HADI DESEMBA , 2024

| | Maelezo | 2024<br>TZS '000 | 2023<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|
| **MALI** | | | |
| Fedha taslimu na akiba katika Benki Kuu ya Tanzania | 19 | 23,398,540 | 25,133,403 |
| Mikopo kwa benki | 20 | 22,730,935 | 22,885,338 |
| Amana za Serikali – Thamani ya Haki Kupitia Mapato Mengine ya Kina (FVOCI) | 23(a) | 10,875,000 | 20,375,253 |
| Amana za Serikali – gharama iliyopunguzwa | 23(b) | 41,538,307 | 32,480,515 |
| Mikopo kwa wateja | 22 | 162,565,818 | 134,261,387 |
| Uwekezajikatika Hisa | 25 | 539,000 | 539,000 |
| Mali ambazo Benki ina haki ya kuzitumia | 26 | 7,046,812 | 8,649,856 |
| Mali nyingine | 21 | 5,054,408 | 4,285,586 |
| Mali na Mitambo | 28 | 5,637,947 | 4,668,883 |
| Mali zisizoshikika | 27 | 1,269,416 | 280,846 |
| Kodi ya mapato ya sasa inayoweza kurejeshwa | 17 | 76,144 | 115,526 |
| Mali ya kodi iliyocheleweshwa | 29 | 1,648,305 | 2,113,717 |
| **JUMLA YA MALI** | | **282,380,632** | **255,789,310** |
| | | | |
| **MADAI NA MTAJI** | | | |
| | | | |
| **Madai** | | | |
| Amana zinazotakiwa kwa Benki | 30(a) | 9,511,626 | - |
| Amana zinazotakiwa kwaWateja | 30(b) | 217,491,606 | 207,396,810 |
| Mikopo ya kuhudumu | 31(a) | 1,508,323 | 1,528,356 |
| Mkopo wa kiwango cha chini cha kipaumbele | 31(b) | 3,119,721 | 2,982,721 |
| Madai mengine | 32 | 2,185,341 | 2,277,088 |
